MKUTANO WA TANO

Kikao cha Pili – Tarehe 13 Oktoba, 2011

Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma dua

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kama kawaida huwatunapata wageni mbali mbali ambao huwa wanakuja ili kuona shughuli za chombo hiki cha wananchi zinakwenda vipi, kwa hivyo leo vile vile tunao wageni ambao ni wanafunzi wa darasa la saba wapo hapa kuja kuona wazee wao wanafanya shughuli kwa ajili yao kwa namna gani, wanafunzi hao idadi yao ni 75 pamoja na walimu wao watano (5) na wanatoka Skuli ya Chumbuni na mwenyewe yupo hapa Mhe. Machano Othman Said Waziri asiyekuwa na Wizara maalum.

Niombe basi wageni wetu hao pamoja na walimu wasimame kwa pamoja ni kura za baadae za Chumbuni hizo. Ahsante sana karibuni sana *(Makofi)*

HATI ZA KUWASILISHA BARAZANI

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais (UUB) (Kny: Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais. Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kuwasilisha taarifa kuhusu tukio la kuzama kwa Meli ya MV Spice Islanders iliotokea tarehe 10/09/2011 katika eneo la mkono wa Bahari ya Nungwi.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Hamza Hassan Juma:(Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa) Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kuwasilisha Hotuba ya ya Maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusu taarifa ya Tukio la kuzama kwa Meli ya MV. Spice Islanders iliyotokea tarehe 10/09/2011 katika eneo la mkono wa Bahari ya Nungwi.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 6

Kufungwa kwa Njia ya Malindi – NBC

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Katika maeneo ya Mji Mkongwe njia inayotokea Malindi kuelekea Benki ya NBC Forodhani na kuendelea ni njia ya kihistoria ambayo ni muhimu sana kwa wakaazi wa Mji Mkongwe na watu wanaofanya kazi katika ofisi zilizopo kwenye maeneo hayo. Katika siku za karibuni, Serikali imeifunga njia hiyo bila ya kutoa sababu zozote, jambo ambalo linaleta usumbufu kwa watumiaji wa njia hiyo.

a) Je, Serikali ina sababu gani za msingi za kuifunga barabara hiyo.

b) Je, Serikali haioni kuwa kuizuia njia hiyo kunadhoofisha huduma muhimu za wakaazi, wafanyakazi na hata watalii wanapotembelea maeneo hayo.

Mhe. Waziri Nchi, (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi – Alijibu:-

Mhe.Spika**,** kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 6 lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, nakubaliana kabisa na Mhe. Mwakilishi kwamba maeneo ya Mji Mkongwe njia inayotokea Malindi kuelekea Benki ya NBC Forodhani na kuendelea ni njia ya kihistoria ambayo ni muhimu sana kwa wakaazi wa Mji Mkongwe na watu wengine wanaofanya kazi katika Afisi ziliopo kwenye maeneo hayo.

Mhe. Spika, kutokana na ongezeko la idadi ya watu na watu wengi kumiliki vipando vya moto katika nchi yetu wakiwemo watu wa Mji Mkongwe, serikali inalazimika mara kwa mara au kila inapoyumkinika kufanya marekebisho ya matumizi ya njia kwa lengo la kupunguza misongamano na kufanya shughuli za wananchi katika mji wetu kwenda kwa ufanisi zaidi bila ya matatizo na bughudha kwa wananchi wetu. Huu ni utaratibu katika Miji yote ulimwenguni.

(a) Serikali haikuifunga barabara inayotoka Malindi na kuelekea Benki ya NBC Forodhani ilichofanya serikali ni kuzuia vipango vya moto kupita kutoka mwisho wa jingo la Ng'ome Kongwe kuingia kwenye dungu la nyumba ya zamani ya watoto wa Forodhani, njia hiyo imefanywa one way na utaratibu huu ni wa kawaida katika miji kwa sababu ya kupunguza misongamano ya magari na vipango vyengine vya moto.

Udhibiti huu una lengo la kuutunza Mji Mkongwe ambao umo katika miji ya urithi duniani, aiza udhibiti huu unafuatia utekelezaji wa *traffic master plan* ya Mji Mkongwe ambao umekubalika kwamba njia inayoanzia Afisi kuu ya Bima Vuga hadi lango kuu la kuingia Bandari ya Malingi iwe ni njia inayopita gari kuelekea Malindi na sivyenginevyo.

(b) Kufunga njia hiyo haitozoofisha huduma muhimu za wakaazi, wafanyakazi na hata Watalii isipokuwa kufanya hivyo kuna imarisha haiba ya Mji wetu na hifadhi ya Mji Mkongwe.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri lakini naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

a) Mhe. Waziri unakubaliana na mimi tokea kufunga njia ile sasa hivi msongamano umezidi zaidi ya mara tatu mpaka nne kuliko ilivyokuwa mwanzo. Vile vile kama ni sababu ya Mji Mkongwe ilikuwa njia kutoka Posta kuelekea Mahakamani ilikuwa imefungwa nayo imefunguliwa sijui kwa sababu gani na kama ni Mji Mkongwe kule kuna majumba mengi zaidi kuliko kule.

b) Kama sikukosea nilivyofahamu kuwa njia kutoka Msikiti wa Malingi mpaka Jumba la kulelea watoto iko wazi umeifungua tayari kwa nilivyokufahamu hivi sasa.

Mhe. Waziri Nchi, (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Sikubali kwamba msongamano umeongezeka, umeongezeka kwa sababu watu tunafanya ukaidi pele kwenye tungu pale la nyumba ya watoto imewekwa kabisa *No entry* kimewekwa kibao kwamba usipite na kiko wazi kabisa lakini mtu kwa makusudi anapita na zamani tulisema kwamba iishie Msikiti wa Malindi, lakini magari yanakuja mpaka Ngome Kongwe kuna *packing* Nzuri ya Forodhani kwa hivyo anaweza kuja mpaka huko hiyo tumeikubali.

Lakini na huku pia tuliruhusu kidogo wakati ule kwa sababu tulipata maombi ya ujenzi na matatizo ya maji katika Mji Mkongwe kwa hivyo kukawa na matatizo ya magari kugeuka tukaruhusu kile kiziwizi pale Afisi ya Wizara ya Nchi Afisi ya Rais Utumishi na Utawala Bora, pia na Afisi ya Wizara ya Ustawi wa Jamii pale tulikiondoa kile kwa muda ule kwa sababu tulipata maombi hayo lakini tuna mipango ya kukirejesha. Kwa sababu hebu tizama msongamano unaotokea mnaviziana kupita kutoka Afisi ya zamani ya Bima mpaka pale na pale kwa taarifa yako wewe huwa unatania na mimi huwa namtania Mhe. Ismail Jussa Ladhu namwambia mtoto wa mjini.

Pale kama unakumbua alikuwa anakaa askari *traffic* pale ili kudhibiti gari kajengewa kistuli kidogo pale kama Mwembeladu, basi alikuwa anasimama pale kwa kuptisha gari zamani, sasa leo tunaviziana njoo usije kwa kweli haipendezi. Kwa hivyo mimi nasema msongamano haupo lakini sote tukubali kutii au kufuata taratibu ziliopo leo kimewekwa usipite lakini mtu utakuta anapita kwa makusudi na kule anapita sasa mnagongana kati kati kwenye tundu haina maana. Kwa hivyo huu ni utaratibu kama nilivyosema watu wanaufanyia utafiti wameona kuna matatizo sasa tuyarekebishe vipi hii ndio njia mojawapo, tunazidi kufanya utafiti tukiona kuna haja basi tutarekebisha.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza suala moja la nyongeza.

Kwa kuwa kuifunga barabara ile kumesababisha msongamano mkubwa katika barabara ile ya Forodhani, jambo ambalo limeleta usumbufu mkubwa kwa wafanya biashara na wafanyakazi, kwa kuwa wafanyakazi ni moja kati ya chanzo muhimu cha uchumi wan

chi yetu kwa kufunga njie ile imekuwa wanachelewa sana kufika kazini pamoja na wafanya biashara ndogo ndogo wa Malindi.

Je, uchumi wa nchi pamoja na uhifadhi wa Mji Mkongwe ni lipi muhimu?

Mhe. Waziri Nchi, (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Naomba nirejee tena unajua ukikosea hili neno moja tu basi huwa unapotosha maana yote, serikali haikuifunga barabara ile, ilichofanya serikali imedhibiti mwenendo wa magari, ukisema kufunga maana yake hakuna kupita ndio kufunga. Lakini tumedhibiti gari zipite kwa mtiririko wa njia moja *one way* na ile njia ya zamani tuue sasa hii ni *one way* kwa hivyo bado hii njia inapitika, lakini hawa wafanya biashara unaowasema katika maeneo hayo na mimi huwa ninakwenda Forodhani pazuri pamenona na kila siku alhamdulillahi panazidi kuchangamka.

Sasa hii inaonyesha mipango tuliyoifanya ya kuwatetea hao wafanya biashara unaowasema kwa sababu ukenda pale hata ile *packing* ya magari kila mmoja anataka kuweka gari mpaka kwenye bustani, sasa kwa utaratibu huu nafikiri mimi ni mzuri kwa *movement* lakini kama nilivyosema serikali inazidi kufanya utafiti ikiona kwamba faida inayopatikana au tija inayopatikana ni ndogo kuliko maudhi basi tutarekebisha hakuna tatizo.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza kama ifutavyo.

Mhe. Waziri alipokuwa akijibu suala la msingi amesema kwamba njia ilivyozuiliwa ni katika tundu lile la jumba la Forodhani, lakini pia ameeleza kuwa njia haikufungwa, kiukweli ni kwamba njia imefungwa kutoka katika Msikiti wa Malindi ndio ilipoanza kufungwa na njia ambayo tunaizungumza ni hii iliyokuwa ikipitwa zanani ambapo gari zinazotokea huku zilikuwa zinapitia katika tundu, na zinazotokea kule zinazunguruka. Sasa zile zinazozunguruka katika hoteli mbele njia ile imefungwa jambo ambalo linasababisha usumbufu wa wafanyabiashara, wafanyakazi na wananchi wote na ndio maana kumekuwa na ulazima sasa wa wananchi kulazimisha kupita katika tundu na wengine wanataka kupita huku na wengine wanataka kuzunguruka.

Lakini pia Mhe. Spika, kwa kuwa Mhe. Waziri katika kikao tulichopitisha taarifa za kamati aliahidi kulishughulikia jambo hilo ikiwemo kuifungua njia hiyo.

Je. Mhe. Waziri ahadi ile ya kuifungua njia ile ili kuondosha usumbufu imeishia wapi?

Mhe. Waziri Nchi, (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mimi nafikiri kwanza naomba kurejea tena neno hili kufunga sasa hivi nimepata labda kilichokusudiwa kumbe ilikuwa ni kufunga kile kipande kile, sasa nasema kwa mujibu wa *Master plan* baadae ramani kubwa kabisa lipo maana yake tunazungumza kwa mantiki iliyopo kwa mujibu wa *master plan* ya Mji Mkongwe hayo ndio mapendekezo yaliyopo.

Sasa kama *Master plan* hiyo unajua imetengenezwa na watu kama tunahisi inaleta kero basi tutakwenda na tutaifuatilia na halafu tutaona nini cha kuirekebisha, kwa hivyo mimi sikatai hii *plan* imefanywa na watu, lakini huo ndio utaratibu uliopo.

Kuhusu ahadi ya kufungua sehemu ile nakumbuka nilisema hilo suala tutalifanyia kazi kwa kwenda kulifanyia utafiti, kuna tatizo gani sasa utafiti nilioufanya kule kunaingia bustanini na tayari kunakera watu wanaopumzika kwa ule upande unaosema. Sasa kupitisha gari kule hapa *fact* chochote kama tutafuta ile ni *one way* hakuna tatizo lilote mimi sioni tatizo, tunachokilalamikia ni mita kumi hadi ishirini tu sasa kama wa Malindi hapiti kuja huku na huku ndio anapita hakuna tatizo lolote.

Mimi nakuomba tukitoka Barazani hapa leo twenzetu mimi na wewe tukafanye utafiti tuone.

Nam. 63

Makaazi Kwa Wafanyakazi

Mhe. Shadya Mohammed Suleiman - Aliuliza:-

Kwa muda mrefu sasa kumekuwa na tatizo la makaazi kwa wafanyakazi wanaopata uhamisho kutoka Unguja kwenda Pemba, hali kadhalika kutoka Pemba kwenda Unguja na familia zao.

(a) Je, Mhe. Waziri, wizara yako ina mpango gani wa kujenga nyumba za wafanyakazi ili kuwaondoshea usumbufu kwa wafanyakazi wanaohamishwa au kuanza kazi.

(b) Je, Mhe. Waziri, Wizara yako ina mpango gani wa kuzifanyia ukarabati nyumba za Serikali ziliopo Tibirinzi Chake-Chake, ambazo kwa sasa ziko katika hali mbaya sana.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 63 lenye kifungu (a) na (b) kama hivi ifuatavyo:-

(a) Hivi sasa wizara yangu ina mpango wa kutafuta wawekezaji kwa ajili ya kujenga nyumba za makaazi na hali tafauti zikiwemo za hali ya juu, ya kati na chini ili kupunguza matatizo ya makaazi kwa wananchi wa hali zote.

(b) Wizara yangu kwa sasa imechukua hatua ya kwashajiisha wakaazi wa nyumba hizo kuzifanyia matengenezo madogo madogo, wizara yangu ina mpango wa kuendeleza sera yake ya nyumba ili kuziuza nyumba hizo au kubaki nazo.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:

Kwa kuwa Mhe. Waziri amesema kwamba serikali ina mpango wa kutafuta wawekezaji kwa ajili ya ujenzi wa nyumba na kwa kuwa miezi michache nyumba Mhe. Waziri wa Wizara hii alifanya safari nchini Qatar pamoja na mambo mengine safari hiyo ilizungumzia pia uwekezaji wa nyumba.

b) Naomba kujua nini kauli ya serikali kwa hatua hii.
c) Uzoefu unaonyesha kwamba kadiri Wizara yako inapopewa jukumu la kugawa nyumba wananchi hudai kuwa kuna upendeleo, kwa mfano ugavi wa nyumba za Michenzani wapo wananchi ambao wanalalamika kuwa kuna upendeleo. Je, hili ni kweli kuna upendeleo au ni kauli za wananchi tu. Na Kama hakuna upendeleo zipo taarifa kwamba zipo nyumba zimebakia kwa nini wafanyakazi hao wasipewe hii leo.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Ni kweli Mhe. Waziri amefanya safari ya kwenda Qatar kwa ajili ya kuzungumza na wawekezaji wa kujenga nyumba za makazi, tayari wawekezaji hao tumeshakubaliana nao na tumeshatiliana saini na tunachosubiri kujipanga kwao na kuja kutekeleza shughuli hizo.

Kasama kwamba kuna nyumba zinagaiwa visivyokuwa kawaida kwa kupewa watu wasiohusika, nataka niseme suala hilo sio kweli nyumba zimegawiwa kwa wale wote ambao wamehusika. Kwanza wamepewa wale ambao wamebomolewa nyumba zao kwa kulipwa fidia na baadae nyumba zilizobakia zimerudishwa Wizarani kwangu wakapewa watu ambao wanahitaji makaazi watu wa aina tofauti hajaangaliwa huyu nani wala huyu nani.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza suala moja dogo tu.

Kuna watu kwa muda mrefu walikuwa wanaishi katika nyumba za serikali nyumba ambazo zilianza kuharibika na kuwa mbovu mpaka zikawa hazikaliki tena, lakini watu hao kwa nia safi na kwa kufuata taratibu zote waliomba kuuziwa nyumba hizo na mpaka leo hawakuuziwa na nyumbe nyengine zimeshaanguka.

Ni sababu zipi hasa za msingi serikali kuanzia watu ambao tokea zamani walikuwa wakikaa katika nyumba zile kuwauzia na kuzitengeneza kwa maslahi yao kuliko zikaachiwa kuanguka hivi na wao wakaachiwa wanahangaika hawana pa kukaa.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Nimejibu kwenye suala mama kwamba wizara yangu inafuata mpango wake wa sera ya nyumba aidha kuziuza nyumba hizo au kubaki nazo, nyumba hizo kwa kipindi cha nyuma nyingi tu tumeziuza na kuwauzia wale watu ambao wanaishi katika nyumba hizo. Kwa hivyo na sasa hivi tutatekeleza mpango huo kwa yule yoyote ambae atahitaji na yule anayeishi katika nyumba hizo.

Nam. 17

Kuanzishwa Vyuo vya Uvuvi Wilayani

Mhe. Abdi Mosi Kombo - Aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ina mkakati wa kufanya Mapinduzi ya Uvuvi na kuwashajihisha vijana kwa wingi kuhusiana na suala hili kama nchi nyengine duniani zinavyofanya.

Je, Mhe. Waziri katika kufanikisha suala hilo Serikali haioni kuwa ipo haja ya kuanzisha vyuo ndani ya Wilaya zetu ili kukuza elimu ya uvuvi kwa vijana wetu.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 17 kama ifuatavyo:-

Kwamba katika kukuza elimu ya uvuvi kwa vijana nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba ipo haja ya kuanzisha Vyuo vya Uvuvi Nchini, na kwamba vijana hao watapohitimu watashiriki vyema katika mkakati wa kufanya Mapinduzi ya Uvuvi Nchini.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, namuuliza Mhe. Waziri kwa kuwa amekubali na kwa kuwa ameona iko haja ya kuanzisha vyuo vya uvuvi kwa ajili ya kuwaelimisha wananchi wetu na kuleta tija katika nchi yetu.

Kwa kuwa visiwa vyetu vya Unguja na Pemba kuna majimbo ambayo ni muhimu sana na yana wavuvi zaidi kama Kojani, Micheweni, Matemwe, Tumbatu n.k na maeneo mengine.

Je, katika kukuza elimu hiyo atakubaliana na mimi kama kuna haja ya kutoa vipaumbele kwa majimbo hayo ambayo yana watu wataalam kama zamani na wanataka kuendelezwa zaidi.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Nakubaliana nae kwamba katika kuanzisha Vyuo vya Uvuvi nchini basi mkazo na kipaumbele yawekwe katika maeneo ambayo wavuvi wengi wanatoka. Nakubaliana na yeye.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuuliza suali la nyongeza la kuweza kumuuliza Mhe. Waziri.

Katika jibu lake mama Mhe. Waziri alikubali kwamba ni kweli kuwa suala hilo ipo haja ya kuweza kuwepo vyuo. Lakini naomba nimuulize je, Mhe. Waziri ni lini mpango huo utakuwa tayari ili wananchi wetu waweze kunufaika kupata taaluma hiyo ya uvuvi.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, nilipokuwa nawasilisha hotuba ya Wizara ya Mifugo na uvuvi mwezi wa Julai mwaka 2011 katika ukurasa wa 40, nilieleza kwamba kwa kuanzia Wizara ya Mifugo na Uvuvi inafanya mazungumzo na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuona namna ya kuanzisha mtaala wa uvuvi katika vyuo vyetu vya Amali vilivyokuwepo Mkokotoni na Vitongoji. Mashauriano hayo yanaendelea vizuri na wakati wowote hali itakaporuhusu basi mtaala huo tutaanzia kwa hapo kanza.

Mhe. Mussa Ali Hassan: Mhe. Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi ya kumuuliza Mhe. Waziri suali moja la nyongeza.

Mhe. Waziri kwa hivi sasa tuna mpango mkubwa wa kuimarisha masuala ya uvuvi. Je, kuna mpango gani wa kuweza kupata vifaa vya uvuvi kwenye majimbo yetu hasa meli za kisasa na nyavu za kisasa, ili kuweza kuendeleza wavuvi.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Nakushukuru Mhe. Spika, ni kweli hivi sasa wizara na serikali kwa jumla imeangalia kwamba shughuli za uvuvi ni shughuli muhimu ambazo zitaweza kuwasaidia wananchi kuondokana na umasikini.

Katika kulitekeleza hilo Wizara yangu inaendelea kuwashajihisha wawekezaji kutoka nje waje wawekeze katika nchi yetu. Katika kufanya hivyo wajenge viwanda vya samaki na pia waanzishe program maalu ya kuwakopesha wavuvi wetu vifaa vya kwenda kuvua. Ambapo wavuvi vifaa hivyo watavitumia kwa kwenda kuvua na baadaye kuiuzia viwanda vya samaki. Ili katika hilo wavuvi wetu watapata faida na pia viwanda vitapata malighafi kwa ajili ya ku – *process* samaki katika nchi yetu.

Nam. 48

Wimbi la Wataalamu Kuondoka Nchini

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Nchi yoyote duniani inahitaji wataalamu katika kupiga hatua kiuchumi na kijamii. Serikali yetu imekuwa ikijitahidi sana kujibana katika baadhi ya mambo ili kusomesha wataalamu wake, lakini kwa bahati mbaya kumekuwa na wimbi la wataalamu hao kutokurudi tena hapa nchini baada ya kumaliza mafunzo au huondoka nchini baada ya muda mchache kurejea masomoni.

(a) Je, Mhe. Waziri huoni kama hii ni hasara kwa Serikali na wananchi kwa ujumla.

(b) Wizara na Serikali kwa pamoja inajiandaa vipi kukabiliana na tatizo hilo.

Mhe. Waziri wa Nchi, (AR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 48 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, suali lake naomba kutoa maelezo ya msingi yanayohusiana na suala hilo.

Kwanza napenda nikubaliane na Mhe. Mwakilishi, kuwa nchi yoyote duniani inahitaji wataalamu ili iweze kupiga hatua kiuchumi na kijamii. Serikali yetu imekuwa ikijitahidi kujibana katika utekelezaji wa baadi ya mambo muhimu ili kusomesha wataalamu wake. Lakini kwa bahati mbaya ni kweli kumekuwa na wimbi la wataalamu hao kutokurudi masomoni bada ya kumaliza mafunzo au kuondoka muda mchache baada ya kurudi masomoni.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hao sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 48 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Wizara yangu na serikali kwa jumla inalifahamu tatizo liliopo na kwamba ni hasara kubwa kwa serikali na Nchi kwa ujumla kwa sababu yale maeneo ambayo yalitaraji wataalamu hao kuja kukabiliana na matatizo au upungufu ulipo na kutoa huduma kwa wananchi yanaendelea kuwa na upungufu na matatizo makubwa. Kwa mfano, nchi yetu bado inaupungufu wa Madaktari Wataalamu wa Kilimo na Mifugo, Wahandisi wa Ujenzi, Miundombinu ya barabara na kadhalika.

(b) Wizara yangu imechukua hatua zifuatazo ili kukubaliana na tatizo hilo:-

Kwanza: Inaandaa mkataba wa masomo ambao vijana watakaopelekwa masomoni watalazimika kuingia katika mkataba wa makubaliano baina yao na Serikali na kuahidi kwamba baada ya kumaliza masomo yao watarudi nchini kuja kuwatumikia wananchi. Vyenginevyo mfanyakazi huyo atalazimika kulipa gharama za masomo kupitia kwa waliomchukulia dhamana hiyo

Pili: Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya awamu ya saba imepandisha mishahara ya wafanyakazi na wataalamu kwa asilimia kubwa kuanzia mwezi huu wa Oktoba 2011, ili kumfanya mtaalamu aweze kubaki na kuendelea kufanyakazi hapa Zanzibar. Lengo la Serikali ni kuhakikisha kwamba mishahara ya Wataalamu wetu haitafautiani mno na mishahara ya wataalamu kama hao wanaotumikia Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Aidha, Mhe. Spika, serikali hivi sasa imeunda Kamati Maalumu itakayofanya utafiti wa masuala ya Ajira Nchini, ambayo pamoja na mambo mengine itaangalia kwa undani zaidi changamoto za ajira nchini kwa wataalamu na watendaji wengine na kupendekeza kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hatua ambazo zinapaswa kuchukuliwa ili kukabiliana na changamoto hizo.

Mhe. Spika, ukosefu wa ajira kwa wataalamu nayo ni changamoto inayopelekea, wataalamu wetu kutorudi nchini baada ya kuona wenzao wenye sifa kama zao ambao wamewatangulia kurudi masomoni bado hawajaajiriwa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Katika suala langu la msingi niliilouliza ni kwamba nchi yoyote duniani inahitaji wataalamu kupiga hatua kiuchumi na kijamii. Dereva nay eye vile vile ni mtaalamu. Wizara ya Elimu imeleta ombi la kumuajiri dereva Skuli ya Kengeja kwa muda mrefu na haijapata jawabu.

Je, unataka kuliambia Baraza hili kwamba hakuna uwezo wa kumlimpa dereva huyo wa skuli ya Kengeja. (*Makofi*)

Mhe. Waziri wa Nchi, (AR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, nimpongeze Mhe. Jaku kwa swali lake zuri la nyongeza aliilouliza.

Mhe. Spika, mtu yeyote mwenye ujuzi wowo ni utaalamu, hata tarishi na ujuzi ule wa utarashi akifanya vizuri na yeye pia ni mtaalamu. Suala lake mama alikusudia hasa wale wataalamu kama Madaktari, Wahandisi na wengineo kama nilivyowataja. Suala la dereva wa Skuli ya Kengeja kama lipo basi wizara yangu kazi yake ni kupokea maombi kutoka wizara husika na hatimaye kuwaruhusu wizara iweze kumuajiri dereva huyo kwa mujibu wa taratibu na sheria za utumishi zilizopo.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante Mhe. Spika, naomba nimshukuru Waziri kwa majibu yake fasaha, lakini naomba nimuulize swali moja la nyongeza.

Mhe. Spika, katika siku za karibuni katika serikali hii ya awamu wa saba yenye muundo wa Umoja wa Kitaifa kumekuwa na wimbi la kuwaajiri watu wastaafu ambao wanaonekana wamechoka na wengi katika nafasi zao walizokuwa wakizitumikia awali hawakuwahi kuonesha ufanisi wowote.

Je, hatuhisi kuwaajiri watu wa aina hii au kuwarejesha kazini kwa namna yoyote ile hakuwavunji moyo wataalamu wetu ambao tumewasomesha kwa pesa nyingi na ambao wanazihitaji nafasi hizi. Pengine wao wangeweza kutoa mchango mkubwa zaidi kuliko wale ambao walipokuwa katika nafasi hizi hawakuonekana kutoa mchango mkubwa kiasi cha kupumzishwa. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Waziri wa Nchi, (AR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, ni kweli serikali yetu imewaajiri baadhi ya watumishi wastaafu katika shughuli au katika baadhi ya maeneo ya taasisi za serikali. Hiyo inatokana na kwamba kama Sheria yetu ya Utumishi wa Umma inavyooeleza kwa yale maeneo ambayo bado yanahitaji utaalamu huo walionao hao wastaafu, basi serikali inatoa kibali kwa ajili ya kuwaajiri wataalamu hao au watumishi hao. Kwa yale maeneo ambayo hayahitaji kabisa utaalamu wa mstaafu huyo basi serikali yetu haifanyi kazi ya kuwaajiri wastaafu.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Katika jibu lake Mhe. Waziri amesema hivi karibuni kuna mshahara umepandishwa kwa ajili ya wataalamu. Atakubaliana na mimi Mhe. Waziri kuwa kupandishwa kwa mshahara ni kidogo na ndio maana ikapelekea wataalamu kutokurudi.

Mhe. Waziri wa Nchi, (AR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, ni kweli kwamba serikali imeamua kupandisha mishahara ya watumishi wake wote wa serikali. Kuanzia mwisho wa mwezi huu wa 10 mishahara hiyo mipya itaanza kupatikana kwa watumishi wote wa umma.

Kwa kiasi Fulani serikali imejitahidi sana kupandisha kupandisha viwango vya mishahara ya wafanyakazi pamoja na wataalamu. Siamini mimi kwamba viwango hivyo kwa mujibu wa hali ya uchumi wetu kwamba ni vidogo. Viwango vya wataalamu na viwango vya watumishi vimetoka kutoka asilimia 25 hadi asilimia 50. Ni imani yangu huu ni mwanzo wa kuanza kuwapandishia watumishi wetu mishahara ili hali zao ziwe nzuri.

Katika hotuba yangu ya bajeti nilisema kwamba utaratibu huu utaendelea mwaka hadi mwaka. Kwahiyo mwanzo ni mzuri na naomba wafanyakazi wote au watumishi wote wa umma wapokee kile ambacho serikali yao imeamua kuwapangia kutokana na hali halisi ya uchumi wa nchi yetu.

Nam. 11

Chelezo cha Bandari ya Malindi

Mhe. Salim Abdalla Hamad - Aliuliza:-

Shirika la Bandari lilijenga chelezo katika bandari ya Malindi. Tokea kuanza kazi kwa chelezo hiyo, vyombo vingi vimefanyiwa matengenezo makubwa ikiwemo M.V. Jitihada ambayo hivi sasa imeshaanza kazi. Kutokana na umuhimu huu,

(a) Kwa nini Serikali haitafakari kwa makini umuhimu wa kuhamisha mali zake kutoka Shirika la Meli na kukabidhiwa Shirika la Bandari ili liweze kutoa huduma na kutunzwa.

(b) Kutokana na umuhimu wa chelezo hiki, Serikali haioni kuwa hivi sasa kuna umuhimu wa kutoa kila msaada kwa Shirika hili ili chelezo hicho kiweze kurefushwa kuelekea kina kikubwa cha maji ili kiweze kuhudumia katika matengenezo ya vyombo vikubwa zaidi vya baharini.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 11 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Shirika la Bandari na Shirika la Meli ni Mashirika mawili yalioanzishwa kwa madhumuni tofauti – Shirika la Bandari limepewa jukumu ya kufanya biashara ya huduma za Bandari ambapo Shirika la Meli limepewa jukumu la Biashara ya Usafirishaji wa abiria na mizigo, pamoja na Uwakala wa Meli za Kigeni. Pamoja na kwamba Shirika la Bandari linaruhusiwa kisheria kufanya biashara ya Usafirishaji kwa njia ya bahari, shughuli zake

za msingi ni kuhudumia meli zinazoingia na kutoka katika Bandari za Unguja na Pemba katika utoaji wa huduma hizo za Bandari hadi sasa Shirika hili linakabiliwa na mahitaji kadhaa, ambayo kimsingi yanahitaji fedha nyingi ili kuliwezesha kutoa huduma zake kwa ufanisi zaidi, hivyo wazo la kuzihamisha mali (Meli) za Shirika la Meli na kukabidhiwa Shirika la Bandari kwa hivi sasa halitoleta ufanisi unaotarajiwa, kwa sababu ili meli za Shirika la Meli ziweze kutoa huduma bora na kufanya kazi vizuri zinahitaji fedha nyingi kwa ajili ya matengenezo.

Mhe. Spika, jambo la msingi ni kwa Mashirika haya mawili ni kushirikiana kwa vile kazi zao zina uwiyano, hata hivyo kwa upande wa Shirika hili la Bandari kama litakuwa na uwezo wa kifedha za kununua meli zake, sheria yao inawaruhusu.

(b) Mhe. Spika, ni kweli kwamba Shirika la bandari lina mpango wa kukirefusha Chelezo kilichopo Malindi zinahitajika fedha nyingi, ili kuweza kukamilisha utekelezaji wa mpango huo. Hata hivyo kwa mpango wa Bandari kipaumbele chao hivi sasa ni kununua vifaa vya kutoa huduma bora zaidi za uwezeshaji na upakiaji wa mizigo katika Bandari ya Unguja na Pemba.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, nashukuru kwa kupata jibu zuri la suala langu. Lakini nina suala dogo la nyongeza. Mhe. Spika, sababu ya kuleta suala hili ni kuwa hata Wizara ya Kilimo ilikuwa ina Meli ya MV. Jitihada, ikaharibika, ikawashinda na serikali ikaipeleka Shirika la Bandari na ikafanyiwa matengenezo mpaka hivi sasa Alhamdulillah inatumika. Tofauti la Shirila la Meli, alipewa meli tatu mpya MV. Mapinduzi, MV. Maendeleo na MV. Ukombozi ya mafuta, zote zimekwenda na wala hatuoni chochote.

(a) Kwa nini hawa wenye uwezo wa kutengeneza hizi meli zinazoharibika hawapewi zikawa zipo imara na kuzalisha nyengine kuliko kupewa hawa.

(b) Kama haiwezekani hayawezi yakaundwa mashirikiano yoyote ikaonekama kuwa kuna mashirikiano mazuri ya kushughulikia hivi vyombo vyetu baina ya Shirika hili la Meli na Shirika la Bandari.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, dhamira ya serikali kama tulivyoeleza ni kurahisisha na kuimarisha huduma za jamii likiwemo suala la usafiri.

Napenda nikiri kwamba ni kweli Wizara ya Kilimo walikuwa wakilimiliki meli hiyo ya MV. Jitihada, serikali wakafanya maamuzi ya kulipatia shirika la Bandari na wameweza kuifanyia marekebisho na hivi sasa inatoa huduma nzuri ya usafiri hasa wa mizigo kati ya Unguja na Pemba.

Maelezo yetu ya awali tumesema kwamba kwa hivi sasa haujawa muda muafaka wa kusema kwamba meli zile tuziondoshe kutoka Shirika la Meli kwenda katika Shirika la

Bandari. Jambo la msingi ni kuona ni kwa kiasi gani mashirika haya mawili yanafanya kazi kwa kusaidiana ili kuweza kupeleka ufanisi unaohitajiwa na wananchi wote.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi hii kumuuliza Mhe. Naibu Waziri suala la nyongeza lenye vifungu (a) na (b).

(a) Kwa kuwa imetajwa katika suala na katika jibu mama kuhusu uwezo wa Shirika la Meli. Je, ni haki kuliita Shirika la Meli ikiwa hakuna meli hata moja inayokwenda.

(b) Na ikiwa si haki kwa nini halifungwi

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, Shirika la Meli limeanzishwa mwaka 1978. Wakati huo lilipokuwa likianzishwa lilikuwa linamiliki mali na linajiendesha. Shirika kama zilivyo taasisi nyengine ambazo zinafanya kazi na zinategemewa kwamba kuwa kuna tija katika kutoa ufanisi na kupata vifaa vya kuendeleza kazi zake.

Kwa bahati mbaya Shirika la Meli limekuwa utendaji wake si mzuri na kumeonekana mali nyingi zilizokuwa zimeanzishwa na Shirika hili zimekufa. Lakini bado nadhani ipo haja na ulazima wa kuwa na Shirika la Meli na kuendelea na Jina hili.

Hata hivyo sisi kama serikali tumedhamiria kwa dhati kurejesha huduma ikiwemo kutafuta vifaa hasa meli na huduma nyengine zitakazoweza kurejesha hadhi na heshima kama ilivyoanzishwa na Shirika hili.

Nam. 31

Uanzishwaji wa Tarehe za Kiislamu

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Katika kujibiwa suala langu kwenye Mkutano wa Tatu (April 2011) wa Baraza la Nane Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria alikubali kimsingi wazo la kuanza kuadhimisha kuanza kwa tarehe ya Kiislam Zanzibar, na kwa swali ambalo limebaki itakuwa ni kufuwatwa tu kwa taratibu. Mpaka sasa inaonekana suala hilo bado halijaamuliwa rasmi na serikali.

(a) Je, Mhe. Waziri anaweza kutueleza kuwa hatua yoyote ambayo wizara yake imechukua kwa ajili ya kulifanyia kazi suala hilo.

(b) Je, kuna mwelekeo gani wa kufanikiwa katika suala hilo au kuna tatizo gani katika kufanikiwa katika suala hilo au kuna tatizo gani katika kulishughulikia.

(c) Na endapo hakuna tatizo lolololote linalokwamisha wazo hilo kutekelezwa, ni lini utekelezaji wake utaanza.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria - Alijibu:-

Mhe. Spika kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 31 kama ifuatavyo:

Mhe. Spika kama nilivyomjibu Mhe. Mjumbe swali lake katika jibu langu la suala Nam. 121 katika kuwa ipo haja ya kuliangalia kwa undani zaidi suala hili la Sikukuu ya mwezi Mosi Muharram. Bado Wizara yangu inaendelea kusema hivyo hivyo, kwamba ipo haja ya kuliangalia kwa undani zaidi, ingawa nafahamu kikamilifu hamu kubwa aliyonayo Mhe. Jaku katika suala hili na hasa kwa tarehe hii anayoiulizia yaani tarehe mosi Muharram

Katika jibu hilo niliahidi kuwa tutafanya utafiti kwa kuzipitia Sheria zetu za Kiislamu pamoja na kuwatumia wataalam wetu na Masheikh wetu, hasa Idara yetu ya Mufti. Nyote mtakubaliana na mimi kuwa ni juzi tu ndio Mhe. Mufti ameteuliwa na kwamba Baraza la maulamaa sasa liko karibu kuundwa. Baada ya kukamilika haya, ndio sasa tunaweza kupata ushauri mzuri kwao na baadaye kuitaarifu Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais kwa ushauri wao na hatua zao muafaka. Hii ni kwa sababu Afisi ya Mhe. Makamo wa Pili wa Rais ndio Wizara inayohusika na Sikukuu za Serikali na sio Wizara ya Katiba na Sheria.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, wakati Mhe. Waziri anajibu suala hili ilisema kuwa serikali inafuatilia, lakini ufatiliaji wake hauwezi kukamilika mpaka awepo Mufti. Lakini alikuwepo Naibu Mufti.

(a) Huoni hili suala kama unataka kuliondosha njiani tu Mhe. Waziri.

(b) Pia ulitueleza kwamba tulifanya utafiti juu ya sheria zinazohusu mambo haya. Je, utafiti huo umefikia wapi.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, serikali haina azma ya kumuondosha njiani mwakilishi yeyote yule. Serikali ina utaratibu wake wa kufuatilia mambo. Nikiri kwamba alikuwepo Naibu Mufti lakini kama Mhe. Mwakilishi anafuatilia ni kwamba Naibu Mufti aliyekuwepo alikuwa hana Baraza la Maulamaa kwa sababu walikuwa wameshamaliza. Wakati ule tusingeliweza kuteuwa Baraza la Maulamaa kwa sababu mteuzi ni Waziri wakishirikiana na Mufti. Mufti alikuwa hayupo na sasa tumempata. Hivi sasa tupo katika hatua ya kuunda Baraza la Maulamaa. Baada ya hiyo tunajua serikali chombo chake kikubwa cha ushauri wa kidini ni Mufti. Kwa hivyo ndio maana nikasema baadaye tutaipeleka Idara ya Mufti kwa kupata ushauri.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa kuweza kumuuliza Mhe. Waziri suala moja la nyongeza.

Kwa kuwa Mhe. Waziri ameshakiri kama kuna haja ya suala hili kulishughulikia na kwa kuwa sasa Mufti ameshapatikana na karibuni Baraza la Maulamaa litaundwa.

Je, Mhe. Waziri atakubaliana na mimi kwamba kuna haja ya kuharakisha suala hili kwa sababu ni suala muhimu kwa ajili ya wananchi wetu wa Zanzibar ili suala hili lipatiwe ufumbuzi.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, nakubali kwamba kuna umuhimu huo. Lakini utaratibu wa Mufti na Baraza la Maulamaa ni lazima ufuatwe. Sisi tutapeleka huko na wao watachukua wakati wao kwa uharaka kuwaelezea na watafanya utafiti. Ukimaliza utafiti kama nilivyosema baada ya wao kunishauri mimi na mimi nitaishauri Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais. Kwa sababu suala la Sikukuu ni suala ambalo Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais ndiyo inayohusika.

Kwa hivyo mimi baada ya kupata ushauri huo lazima niishauri Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais, nimuandikie na yeye tena ndio mwenye mamlaka ya kuamua.

Nam. 4

Posho la Walimu

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa - Aliuliza:-

Kwa mujibu wa taratibu za kiutumishi katika utumishi wa umma, mwalimu yoyote anayeishi umbali mkubwa kutoka kituo chake cha kazi, hupaswa kulipwa nauli. Pia mfanyakazi anapotakiwa kusafiri kikazi baina ya visiwa vyetu pia hupaswa kulipwa nauli na posho ya kujikimu safarini.

Walimu walioajiriwa na serikali hawana tafauti na wafanyakazi wengine ambao wananufaika na taratibu hizi. Lakini la ajabu ni kuwa kuna kundi kubwa la walimu walioajiriwa na serikali ambao hawalipwi nauli za kwenda na kurudi kazini kwa kisingizio cha kuwa wamejaza mikataba ya kuwa wasilipwe.

Vile vile kwa kipindi sasa walimu wanaochaguliwa kushiriki katika maadhimisho ya siku ya walimu duniani na tamasha la elimu bila malipo, wanapopaswa kusafiri kutoka kisiwa kimoja kwenda kisiwa chengine, hutakiwa kujilipia nauli na pia huwa hawalipwi posho zao stahiki kama wafanyakazi wengine.

(a) Mhe. Waziri anaweza kulifahamisha Baraza hili tukufu, ufafanuzi wa kisheria unaohalalalisha mkataba wa kazi, unaokiuka kanuni za sheria za kazi zilizopitishwa na Baraza hili.

(b) Mhe. Waziri, haoni kuwa kwa serikali inayofuata maadili ya utawala bora, kutoa mkataba wa kazi unaopingana na kanuni za sheria kwa waajiriwa wake, kuwa ni doa, na watendaji wanaosimamia hilo kuwa wanapaswa kuwajibishwa.

(c) Mhe. Waziri, anaweza kulifafanulia Baraza hili, uhalali wa kisheria wa kutokuwalipa posho za kujikimu na nauli walimu wanaotakiwa kusafiri

kikazi wakati wa maadhimisho ya sherehe mbali mbali zinazoandaliwa na Wizara kutoka kisiwa kimoja kwenda kisiwa chengine.

(d) Je, Mhe. Waziri, anaweza kulieleza Baraza hili tukufu, vitendo hivi ambavyo ni kinyume na sheria na taratibu za utumishi, vitaendelea mpaka lini.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:-

Mhe. Spika kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 4 lenye vifungu (a), (b), (c) na (d) kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, ni kweli kuwa serikali imeweka utaratibu wa kuwalipa posho na usafiri wafanyakazi na watumishi wake wote wakiwemo walimu. Posho hili la usafiri limeingizwa katika mishahara ya watumishi wote wa umma. Mbali na posho la usafiri baadhi ya walimu wetu wanalipwa nauli halisi ya usafiri kutokana na kufanya kazi maeneo ya mbali na wanapoishi.

Utaratibu huu ni fursa iliyotolewa kwa walimu tu na sio kwa kada nyengine zilizopo kwenye utumishi wa umma, ambapo baadhi ya wafanyakazi katika sehemu zilizo mbali mbali na sehemu ambazo wanaishi hawalipi nauli halisi kwa mujibu wa masafa wanayosafiri. Kwa hivyo, baadhi ya walimu wetu hawalipwi nauli halisi kwa sababu walipoajiriwa walithibitisha kwa maandishi kuwa ni wenyeji wa maeneo waliyoomba na kupangiwa kazi, na pia hawakuhitaji nauli ya kwenda kazini.

Mhe. Spika, kuwa wenyeji wa eneo mwalimu alipopangiwa kazi ilikuwa ni moja wapo ya sharti ya kupatiwa ajira katika maeneo ambayo yalikuwa na upungufu mkubwa wa walimu na serikali ilitoa kipaumbele kwa ajira katika sehemu hizo. Vile vile kwa mujibu wa utaratibu wa utumishi wa umma, mfanyakazi anaposafiri kikazi anastahiki kulipwa nauli na posho ya kujikimu.

Ni kweli kuwa walimu kama watumishi wengine wa umma wanastahiki kulipwa posho la kujikimu wanaposafiri nje ya sehemu zao za kazi kama hawapatiwi huduma za malazi, chakula na huduma nyengine. Walimu wanaposafiri kwa ajili ya kushiriki maadhimisho ya tamasha la elimu bila ya malipo, siku ya walimu duniani kutoka Unguja kwenda Pemba au Pemba kwenda Unguja wamekuwa wakilipwa nauli, malazi, chakula na posho la shilingi 30,000/= kwa huduma nyengine.
Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo naomba kujibu kama ifuatavyo:-

a) Mikataba ya kazi kati ya wizara na watumishi wake ni mikataba ya kawaida kama ilivyo ya watumishi wengi wa Serikali haikiuki kanuni za sheria za kazi. Hakuna ufafanuzi wa kisheria unaoruhusu kukiukwa Kanuni za Sheria za kazi.

b) Kama nilivyosema kuwa wizara haina mkataba wa kazi na watumishi wake wanaokiuka kanuni za sheria za kazi. Baadhi ya walimu kutolipwa posho la

usafiri hakukiuki kanuni za sheria ya kazi kwani hakuna kifungu cha sheria kinachotaka wizara iwalipe walimu posho la usafiri bali ni fursa tu iliyotolewa kwa walimu. Huu ni utaratibu uliobuniwa na wizara wenyewe katika kuwarahisishia walimu wanaofundisha skuli za mbali kufika kazini kwa wakati. Napenda ieleweke wizara ina watumishi wengi wasiokuwa walimu ambao wanaishi mbali na maeneo ya kazi, na hawalipwi nauli halisi isipokuwa wanapata posho la usafiri linaloingizwa katika mishahara yao.

c) Hakuna uhalali wa kisheria wa kutowalipa wafanyakazi posho za kujikimu na nauli wakati mfanyakazi anaposafiri kikazi. Wizara yangu inalizingatia hilo na wafanyakazi wanaosafiri kikazi kuhudhuria sherehe za kitaifa kama Tamasha la Elimu bila ya malipo, Siku ya Walimu Duniani hulipwa nauli. Pia hupatiwa makazi na malazi na posho la shs. 30,000/= ambalo linakubalika kisheria.

d) Wizara yangu inafuata na itaendelea kufuata kanuni za utumishi wa umma katika kuwahudumia watumishi wake na kamwe haitokubali
kukiuka taratibu zilizowekwa kwani kufanya hivyo ni kwenda kunyume na maadili ya kazi.

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa: Ahsante Mhe. Spika, naomba kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali dogo la nyongeza. Je, hamuoni kutowalipa pesa zao zote shilingi 70,000/= kuwa mtawasumu na kwa nini muwapangie sehemu ya kulala.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, ni kweli posho halisi ya mfanyakazi ni shilingi 70,000/= lakini nataka ieleweke kama posho zinalingana na mahala gani ambapo unatakiwa kwenda kufanya kazi, tuseme kama Unguja na Pemba au Unguja na Dar es Salaam. Lakini ni kwamba inatofautiana na ngazi ya mpewa posho mwenye, hivyo kutokuwalipa posho la shilingi 70,000/= walimu wetu sio kukiuka sheria wala sio kuwadhulumu. Ni kwa sababu tunawalipia nauli, tunawalipia malazi, tunawapa chakula na halafu tunawapa na shilingi 30,000/=. Kwa hivyo, mimi sifikirii kama tunawadhulumu walimu hawa, tunalofanya sisi ni sawa Mhe. Spika.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii nimuulize Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Waziri alipokuwa akijibu swali la msingi amesema kwamba fedha hizi zinazotolewa na Wizara ya Elimu ni fursa tu ambayo inatolewa na sio sheria.

Je, Mhe. Waziri atakubaliana na mimi kwamba fursa ambazo zimezoeleka kutolewa kila wakati zinabakia kuwa sheria, sheria hiyo lazima itekelezwe.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, ni kweli nilipojibu swali mama nilisema kama hizi ni fursa, na sheria pia nilieleza kuwa ni ile ambayo wanalipwa moja kwa moja kwenye mshahara wao. Na fursa hizi ambazo zinatolewa pia nilizieleza kama ni kwa walimu maalum ambao wako mbali na maeneo ambayo wanafanyia kazi.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Spika, nakushukuru sana kunipa fursa kuniuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, Mhe. Waziri alipokuwa akijibu swali amesema kama walimu wanaolipwa nauli kutokana na kusomesha maeneo ya mbali na vituo vyao, basi ameseme kama maposho hayo ya nauli huingizwa katika mishahara yao.

Mhe. Waziri kwa sababu walimu ni kama wafanyakazi wengine kama madaktari huwa wanahamishwa kutoka maeneo haya na kupelekwa katika skuli nyengine kusomesha na maeneo yao yakiwa ni mbali na maeneo wanayokaa na wakati posho zao zinaingizwa katika mishahara. Je, anapohamishwa mwalimu na wakati huku nyuma aliweka mkataba wa kuwa yeye anasomesha katika maeneo ya karibu asilipwe, na wakati sasa akahamishwa eneo jengine la skuli.

Je, anapohamishwa katika eneo jengine na wakati anasomesha mbali na kuna mkataba, huu mshahara wake anaopewa na wakati posho lile lilikuwa limeingizwa pale na sasa hivi halimo. Hivyo, wizara yake inafanya jitihada gani ya mwalimu yule kumlipa posho lake na wakati mkataba wake unaonesha kama hakuingiziwa kwa sababu alikuwa anasomesha karibu. Na je, wizara yake inamlipa kama hamlipi je, inafanya nini wizara yake kuhakikisha mwalimu yule anapata posho lake.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, hapa nilieleza kuna mambo mawili tofauti. Kuna posho ile ambayo ni haki ya mfanyakazi yeyote wa serikali, hiyo ni mbali na ndio ambayo anatiliwa katika mshahara. Posho nyengine ambayo nimeieleza ni ile posho maalum ambayo tunawatiliwa walimu wetu wanaofanya kazi mbali na sehemu ambazo wanaishi, hivyo ikiwa kama mwalimu katika mkataba wake wa mwanzo alieleza kama mimi kwa mfano ni mwenyeji wa Matemwe na nitasomesha skuli ya Matemwe, na ikatokea kwa sababu moja au nyengine, wizara itamuhamisha. Ni kwamba utaratibu utafuatwa na analipwa posho lake kama kawaida Mhe. Spika.

Nam. 40

Mafunzo kwa Ajili ya Viongozi wa Vijana

Mhe. Farida Amour Mohammed (Kny: Mhe. Fatma Mbarouk Said) - Aliuliza:-

Kutokana na mwamko wa vijana wetu kujikusanya pamoja kwa manufaa ya nchi yetu miongoni mwa vijana hao ni viongozi wa wenzao katika vikundi hivyo.
Je, Serikali ina mpango gani kuwakusanya vijana viongozi kwa lengo la kuwapa taaluma ya uongozi ili isaidie kuwaongoza vyema wafuasi wao.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria (Kny: Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto) - Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 40 kwa pamoja kama ifuatavyo:

Mhe. Spika kwa nyakati tofauti wizara yangu imekuwa ikiandaa mafunzo kwa viongozi wa vijana na hasa taasisi za kiraia za vijana juu ya usimamizi wa miradi wa miradi na

vikundi vyao ili kuona shughuli za vijana zinaenda vizuri. Aidha, mafunzo kwa vikundi vya vijana yanahitajika kwa wingi kuliko uwezo wa wizara ilionao kwa sasa, hata hivyo tunawashauri viongozi wa vikundi vya vijana kutumia fursa ziliopo za mafunzo yanayotolewa na taasisi za kiraia nchini pamoja na zile tunazotoa wizarani ili waweze kunufaika zaidi.

Mhe. Spika, wizara itaendelea kutoa mafunzo kwa viongozi wa vijana kila hali na fursa itakapopatikana. Mipango hii pia tumeiweka katika bajeti hii na tumeshaanza kuandaa mipango yetu ya kutoa elimu inayohitajika.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa tena nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa kuna vijana ambao tayari wameshajikusanya katika majumba mbali mbali ya Unguja na Pemba maarufu SOBA HOUSE hawa tayari vijana wameondokana na suala zima la mambo ya kuvuta unga na tayari wameshaanza kujirekebisha tabia zao na wako tayari kuweza kupewa taaluma ili kuendeleza nchi yetu. Je, serikali imeshawahi kusaidia hizi SOBA HOUSE angalau hawa vijana kuweza kupata taaluma na kuweza kujikimu katika nyumba hizi.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria (Kny: Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto): Mhe. Spika, naomba Mhe. Mwakilishi afahamu kwamba serikali ina utaratibu wake na ina ugawaji wa shughuli katika serikali, suala la SOBA HOUSE pamoja na vijana wanaokaa huko ni suala la Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais. Kwa hivyo, utaratibu wote wanaoshughulikia suala hili ni Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais na sio wizara yangu. Hata hivyo, ni suala ambalo tunaweza tukashauriana na Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais ili tuweze kuwasaidia vijana hao.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Waziri hivi sasa kwenye majimbo yetu vijana wengi wamekubali wito wa serikali wa kujikusanya kwa njia ya vikundi vikundi na kwa muda mrefu sana na hivi sasa viongozi ambao wenye vikundi hawajapata mafunzo. Je, hilo Mhe. Waziri unalijua na kama unalijua ni lini viongozi hawa wa vikundi wataweza kupata mafunzo ili kuendesha vikundi vyao visiporomoke.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria (Kny: Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto): Mhe. Spika, nilijibu katika jibu langu mama, nilisema kwamba serikali inajua lakini napenda hapa niwashukuru vijana kwa sababu ni wengi sana waliojitokeza. Hivi sasa vijana waliojitokeza kwa kweli ni wengi ni zaidi ya uwezo wa wizara. Hata hivyo, baadhi tumeshaanza kuwapa mafunzo hayo, wengine tumeshaweka katika mpango wetu, lakini pia kuna mashirika ambayo yanasaidia vijana hawa. Mhe. Spika, ombi langu ni kwamba tushirikiane sote hayo mashirika pamoja na wizara ili vijana wetu tuweze kuwapa mafunzo hayo kwa ukamilifu, na tutaendelea kufanya hivyo.

Nam. 19

Hifadhi ya Maisha ya Wasanii wa Vikundi vya Mila na Utamaduni

Mhe. Abdi Mosi Kombo - Aliuliza:-

Katika nchi yetu kuna vikundi vya mila na utamaduni ambavyo ndani yake wamo wasanii mbali mbali ambao huitangaza nchi yetu na kuipatia umaarufu.

Je, serikali ina mpango gani juu ya wasanii hawa ya kuwahifadhi maisha yao wakati wanapostaafu kazi.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 19 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, bila shaka Serikali ina mpango wa kuhifadhi maisha ya wasanii wakati wanapostaafu kwa njia mbali mbali. Ingawa ukweli usiofichika kuwa kila mtu anayodhima ya kuangalia maisha yake mwenyewe wakati wa kustaafu. Hata hivyo, nafasi ya Baraza la Sanaa na Kamisheni ya Utamaduni na Michezo kwa jumla ni kuwaenzi, kuwaendeleza na kuwashauri wasanii ambao wamesajili katika chombo hicho cha Baraza.

Mhe. Spika, pamoja na kuwapatia ushauri na mafunzo tunawashajiisha wasanii mmoja mmoja au kwa makundi kusajili kazi zao katika Jumuiya ya Hakimiliki Zanzibar (*COSOZA*). Kupitia Jumuiya ya Hakimiliki maisha yao ya kustaafu yanadhaminiwa huko na hata wanapofariki familia zao zinafaidika na kazi hizo kwa muda wa miaka 50 baada kifo cha msanii na hiyo ni njia nzuri ya kuhifadhi maisha ya wasanii wanapostaafu na hata baada ya vifo vyao. Kinyume na hayo hatuna jibu la mkato la kudhamini maisha ya wasanii ila itategemea uwezo wa utundu wao wa kujipatia kipato huku wakila na kubakisha kama wanavyofanya watu wa tathnia nyengine.

Mhe. Spika, kutokana na hali hiyo inatupasa sote tuwe washauri wazuri wa wasanii kuwataka wabadilike kutokana na kazi za kijungujiko wawe wasanii wenye mtazamo wa kisasa kama walivyo wasanii wengine wa nje na ndani ya Tanzania.

Mhe. Abdi Mosi Kombo: Mhe. Spika, napenda kumuuliza swali moja la nyongeza. Je, ni wasanii wangapi waliosajiliwa katika wizara yake.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, ni wasanii 121.

Mhe. Ali Salim Haji: Mhe. Spika, ahsante na mimi kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, katika majibu yake Mhe. Naibu Waziri amesema kwamba hakuna jibu la mkato la kuweza kuwasaidia wasanii hao hivi sasa. Je, haoni kuna haja ya kuwashajihisha wasanii hao kuunda chombo ambacho kinaweza kuwasaidia katika kupata maslahi yao au kuweza kujiwezesha baada ya kustaafu.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, namwambia Mhe. Mwakilishi kuwa swali lake tutalifuatilia na tutalichukulia hatua zinazofaa.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi hii. Mhe. Spika, Mhe. Naibu Waziri alipokuwa akijibu amejigamba sana kwamba serikali inawaenzi wasanii na kwamba hutoa huduma hadi kufariki. Hivi karibuni dunia imemchagua professa Mohammed I-lyas kuwa mshindi wa tatu kidunia katika fani hii ya muziki wa taarab na huko alipata fedha na nishani kubwa kubwa.

a) Je, naomba kujua wao kama wizara walimpa nini.

b) Kwa kuwa amesema kwamba wasanii wanaenziwa naomba kujua zawadi ambazo wasanii angalau wanne hapa Zanzibar wamepewa.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, kwa kweli niseme kwamba kwa upande wa wizara tulikuwa hatuna chombo madhubuti ambacho cha kuwatunza wasanii, na ndio maana tukaja na chombo cha *COSOZA* kwa makusudi kwa sababu tulikuwa tunafanya kazi za wasanii kimazoea. Kwa hivyo, tumeunda hii *COSOZA* ili wasanii wote waweze kujisaidili katika *COSOZA* kwani ndio inayowashajihisha, ndio inayowapa mafunzo na ndio kama bima yao, ili msanii anapofariki basi huwa anapata malipo yake.

Mhe. Spika, ndio maana tukasema kuna vikundi 24 vilivyojisajili pamoja na wasanii 121. Kwa hivyo, lengo na madhumuni ni kuwashajihisha na kuhakikisha kwamba msanii anapofariki basi familia yake iwe inapata mafao yake, hao waliopita ilikuwa wanafanya kazi kwa mazoe. Lakini kulikuwa hakuna chombo maalum cha kuweza kuwatunza ndio maana tukasema lazima wasanii wote wajisajili.

KAULI YA SERIKALI

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kabla sijamwita Mhe. Makamo wa Pili wa Rais nataka nitoe maelezo kidogo kuhusiana na kauli ya serikali. Utakapoangalia kanuni inayohusu kauli ya serikali kanuni ya 43, kitu kauli ya serikali huioni, isipokuwa utaona kauli za mawaziri na mawaziri ukiangalia tafsiri zake kwenye kanuni ya pili ya 2 zetu za Baraza huoni Makamo wa Pili wa Rais.

Kwa hivyo, utakuta kwamba huko nyuma kabla ya mfumo huu wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa tulikuwa na Waziri Kiongozi ambaye yeye ndiye aliyekuwa Mkuu wa Shughuli za Serikali ndani ya Baraza hili. Kwa hivyo, baada ya mfumo huu nafasi hiyo imeondolewa na badala yake ipo nafasi ya Makamo wa Pili wa Rais. Hatukuwahi kuzingatia vizuri ili kila pale ambapo kulikuwa na nafasi ya Waziri Kiongozi kwa shughuli zake tukaingiza Makamo wa Pili wa Rais.

Kwa hivyo, kwenye kanuni hii ya 43 ambapo tunataka kutoa kauli ya serikali, haidhuru kimaudhui kanuni hiyo ile kauli ya mawaziri ndio kauli wenyewe ya serikali, kwa sababu

mawaziri ni mawaziri wa serikali. Sasa kwa watunga sheria aghlabu huwa tunataka kila jambo liwe limetajwa *specifical*, kwa hiyo hii haiko *very specific* chini ya kanuni ya 43 ya kauli za mawaziri, kwamba ndio kauli ya serikali. Kwa mamlaka niliyopewa chini ya ibara ya 153 linapotokea jambo la aina hii ambalo haliko wazi katika kanuni basi Spika anaweza kuelekeza utaratibu utakaotumika juu ya jambohilo. Na kwa sababu serikali kwa hapa shughuli zake imesimamiwa na Makamo wa Pili wa Rais ndio pia tunayemtegemea atoe kauli ya serikali katika chombo chetu hiki.

Kwa hivyo, kwa mamlaka niliyopewa chini ya kanuni hiyo ya 153, kanuni hii ya 43 pia ichanganywe pamoja na kauli ya serikali ambayo itatolewa na Makamo wa Pili wa Rais. Baada ya maelekezo hayo sasa nimuombe basi Mhe. Makamo wa Pili wa Rais kutoa hiyo kauli ya serikali.

TAARIFA KUHUSU TUKIO LA KUZAMA KWA MELI YA *MV. SPICE ISLANDERS* ILIYOTOKEA TAREHE 10/09/2011 KATIKA ENEO LA MKONDO WA BAHARI YA NUNGWI

Mhe. Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, awali ya yote na mimi niungane na wenzangu waliotangulia kuzungumza kwa kutoa pole zangu za dhati kwa familia na jamaa wa marehemu Maalim Mussa Khamis Silima kwa kufiwa na mpendwa wao Mhe. Maalim Mussa Khamis Silima ambaye alikuwa mwenzetu katika Baraza hili, tumuombe Mwenyezi Mungu ailaze roho yake mahali pema peponi. Amin.

Aidha, napenda kutoa pole zangu za dhati kwa famili zote zilizoathirika na ajali ya meli ya *MV. Spice Isla*nders iliyotokea tarehe 10/09/2011 Mwenyezi Mungu awape moyo wa subra wale wote waliopotelewa na wapendwa wao na kuwaombea malazi mema peponi wale wote waliofariki.

Mhe. Spika, kwa heshima kubwa naomba kutoa tamko la serikali na kauli ya serikali kuhusu tukio la kuzama kwa meli ya *MV. Spice Islanders* iliyotokea tarehe 10/09/2011 katika eneo la mkondo wa bahari ya Nungwi.

Mhe. Spika, kwa heshima naomba kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kukutana hapa tukiwa wazima na wenye afya

Mhe. Spika, kwa heshima naomba kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kukutana hapa leo tukiwa wazima na wenye afya njema na kutuwezesha kuendelea na kikao cha pili cha Mkutano wa Tano wa Baraza letu tukufu. Pili naomba nichukue nafasi hii adhimu kukushukuru wewe Mhe. Spika, kutupatia fursa hii adhimu ili kuwasilisha mbele ya Baraza lako tukufu kauli ya serikali kuhusu maafa ya kuzama kwa Meli ya *MV. Spice Islanders* iliyotokea katika mkondo wa bahari ya Nungwi tarehe 10 Septemba, 2011.

Mhe. Spika, Meli ya *MV. Spice Islanders* ilitengenezwa mwaka 1974 nakufanyiwa marekebisho makubwa nchini Ugiriki mwaka 2001. Meli hii ilinunuliwa na *Visiwani Shipping Comapany* mwaka 2007 na kupatiwa usajili tarehe 10/10/2007 baada ya

kufanyiwa ukaguzi kwa mujibu wa Sheria ya Usafiri Baharini ya mwaka 2006 na iliruhusiwa kubeba abiria 600 na mizigo tani 500. meli hiyo ina urefu wa mita 58.15 na upana wa mita 11.4

Mhe. Spika, mnamo tarehe 10/09/2011 majira ya sa nane na tisa za usiku ilipatikana taarifa ya ajali ya kuzama kwa meli hiyo katika maeneo ya mkondo wa bahari ya Nungwi. Meli hiyo ilikuwa katika safari yake ya kawaida ya kutoka Unguja kwenda Pemba ikiwa imebeba abiria na mizigo. Awali, meli hiyo iliondoka bandarini ya Dar es Salaam mnamo saa 5 za asubuhi siku ya tarene 9/9/2011 ikiwa imebeba mizigo na abiria kuelekea Wete Pemba kupitia Unguja. Kwa mujibu wa taarifa za Mamlaka ya Bandari Tanzania, meli hiyo ilikuwa na jumla ya abiria 229 (kati yao watoto 63) na mizigo tani 58. Abiria 136 walitokea Dar es Salaam walikuwa wanaendelea na safari yao hadi Wete Pemba.
Kwa mujibu wa taarifa ya Mamlaka ya Usafiri Baharini (*Zanzibar Maritime Authority*), meli hiyo imeondoka Unguja kuelekea Wete Pemba majira ya saa 3:20 usiku wa tarehe 9/9/2011 ikiwa imepakia abiria 610 na mizigo tani 95.

Taarifa hii inaelezea kwa kina juu ya hali halisi ya tukio pamoja na hatua zote zilizochukuliwa kuanzia tarehe 10/9/2011 hadi hivi sasa.

Mhe. Spika, mara baada ya tukio hili Kamati ya Kukabiliana na Maafa ya Taifa ilikutana usiku huo huo kwa ajili ya kuweka mikakati ya hatua ya kuchukua pamoja na kuandaa taarifa rasmi ya serikali kwa wananchi kupitia vyombo vya habari. Aidha, Baraza la Mapinduzi lilikaa na kutoa maagizo juu ya hatua ya kuchukua ikiwemo kutayarisha eneo la Maisara kwa ajili ya mapokezi na utambuzi wa maiti, kutayarisha eneo la kuzima miili ya marehemu huko Kama; kuweka takwimu sahihi za majeruhi na waliofariki katika ajali hiyo; pamoja na kutolewa kwa taarifa rasmi ya hali ya maafa.

Vile vile Baraza hilo liliagiza kutangazwa kwa siku tatu za maombolezo kuwa na siku maalum ya dua ya kitaifa kwa ajili ya waliofariki; kuundwa kwa kamati ya viongozi ya kuzifariji familia zilizopoteza ndugu na jamaa zao na kuweka utaratibu mzuri wa kuratibu misaada na michango inayotolewa.

HATUA ZILIZOCHUKULIWA

Kufuatia maagizo hayo ya serikali hatua zifuatazo zilichukuliwa:-

- Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi siku ya tarehe 10/9/2011 alilitangazia rasmi taifa kuhusu tukio la kuzama kwa meli ya kuwa taifa liko katika hali ya maafa pamoja na kutanaza siku tatu za maombolezo.
- Vituo vya mapokezi ya wahanga wa ajali hiyo vilifunguliwa katika maeneo ya Bandari ya Malindi, Nungwi na Maisara kwa Unguja. Kwa upande wa Pemba vituo vilifunguliwa katika maeneo ya Bandari ya Mkoani, Uwanja wa Gombani Chake Chake na Ukumbi wa Jamhuri, Wete.
- Vikosi vya Ulinzi na Usalama vilipelekwa katika maeneo mbali mbali ili kuimarisha huduma za ulinzi na uokozi wa haraka.

- Kazi ya uchimbaji wa makaburi katika eneo la Kama ilifanyika kwa mashirikiano makubwa ya viongozi wa Mkoa wa Mjini na Magharibi, Vikosi vya Ulinzi na Usalama pamoja na wananchi. Jumla ya makaburi 134 yalichimbwa.
- Sala na dua maalum ya kuwaombea marehemu wote ilifanyika baada ya Sala ya Alasiri tarehe 12/9/2011 katika viwanja vya Maisara. Katika sala hiyo wagonjwa waliombewa kupata nafuu ya haraka na wafiwa kuwa na moyo wa subira.
- Kuorodhesha majina ya wale wote ambao wanasadikiwa walikuwemo ndani ya chombo kilichopata ajali na hadi sasa hawajuliikani walipo. Taarifa hizi zinakusanywa kupitia ngazi ya shehia na wilaya kwa Unguja na Pemba.
- Kutoa huduma ya kuwasafirisha majeruhi baada ya kupata matibabu kurudi makwao
- Kutoa huduma za chakula na usafiri kwa walioshiriki katika shughuli nzima ya uokoaji.

MATOKEO YA UOKOAJI

Mhe. Spika, kutokana na shughuli ya uokoaji iliyofanywa na vikosi vya ulinzi na usalama kwa mashirikiano makubwa ya wananchi hasa wa maeneo ya Nungwi yamepelekea kuwa na idadi ya watu waliyookolewa wakiwa hai kufikia 619 na miili ya waliofariki dunia iliyopatikana kufikia 203. kati ya maiti hizo 197 zilipokelewa kituo cha Maisara na 5 zilipatikana na kuzikwa Mombasa Kenya na moja ilipatikana na kuzikwa Moa, Mkoani Tanga. Mpaka hivi leo hakuna taarifa yoyote ya kupokelewa kwa miili zaidi.

Kwa waliyookolewa wakiwa hai waliweza kufikishwa katika Hospitali ya Kivunge, Hospitali ya Jeshi Bububu na Hospitali ya Mnazi Mmoja kwa uchunguzi na matibabu. Majeruhi wawili kutokana na hali zao walisafirishwa na kupelekwa katika Hospitali ya Muhimbili. Hadi sasa majeruhi wote wameshatibiwa na kuruhusiwa.

Mhe. Spika, katika kituo cha Maisara maiti zilipangwa ili kuwawezesha ndugu na jamaa kutambua maiti wao na kwa kurahisisha kazi hiyo, Shirika la Utangazaji kupitia kituo chake cha Televisheni na *Zanzibar Cable Television* walichukua picha za sura za marehemu na kuzionyesha zikiwa tayari zimewekewa namba ili kurahisisha utambuzi na uchukuaji wa maiti hao. Kupitia utaratibu huu, jumla ya maiti 158 zilitambuliwa na kukabidhiwa jamaa na ndugu zao kwa ajili ya mazishi. Idadi ya maiti ambazo hazikutambuliwa ni 39 na mazishi yao yalisimamiwa na serikali katika eneo la Kama. Kila maiti alizikwa katika kaburi lake chini ya usimamizi wa mashekhe kutoka Ofisi ya Mufti na Wakfu na Mali ya Amana. Jumla ya maiti 6 ambao hapo awali walitambuliwa na jamaa zao pia walizikwa katika eneo la Kama na hivyo kufanya jumla ya maiti waliozikwa katika eneo hilo kuwa ni 45.

Aidha, katika kituo cha Maisara huduma za uoshaji na sala za maiti zilitolewa na pia wale wote waliochukua maiti walipatiwa sanda na ubao kwa ajili ya kuzikia.

Juhudi za kutafuta meli na watu waliokuwa hawajaonekana

Mhe. Spika, katika jitihada za serikali za kuhakikisha miili zaidi za marehemu waliotokana na ajali ya meli inapatikana, serikali ilipata msaada wa wazamiaji kutoka Afrika ya Kusini. Hivyo, siku ya Jumatatu tarehe 12/9/2011 Kikosi cha Jeshi la Wanamaji kutoka Afrika ya Kusini kiliwasili Zanzibar kwa ajili ya kusaidia shughuli za uokoaji katika eneo la tukio. Kikosi hicho kilikuwa na jumla ya askari 22 wakiwemo wazamiaji 12, wahudumu wa afya 4 na wahudumu wa ndege 6. aidha, kikosi hicho kilikuja na vifaa mbali mbali vya uokozi.

Asubuhi ya tarehe 13/9/2011 wazamiaji hao kwa kushirikiana na Jeshi la Wananchi wa Tanzania na kikosi cha KMKM walifika katika eneo la tukio kwa ajili ya kuanza kazi rasmi. Hata hivyo, wazamiaji hao walishindwa kufanya kazi zao kutokana na kina kirefu cha maji katika eneo hilo ambacho kinakadiriwa kuwa kati ya urefu wa mita 279 hadi 300. Vile vile kwa siku hiyo eneo hilo lilikuwa na mawimbi makali na mwendo wa kasi wa maji ambapo ilisadikiwa kwamba ilikuwa unakwenda *(water drifting 4 miles for hours)*. Aidha, vifaa walivyokujanavyo wazamiaji hao ni vile vilivyoweza kutumika si zaidi ya kina cha maji mita 80 tu.

Mhe. Spika, vikosi hivyo viliendelea na jitihada za kutafuta meli na watu waliokuwa hawajaonekana na kujigawa katika makundi matatu. Makundi mawili yalihusika na kazi ya utafutaji wa watu katika maeneo ya ukanda wa eneo la tukio kuelekea upande wa kaskazini ambao ni Pangani na Ghuba ya Moa Mkoa wa Tanga. Kundi jengine lilijihusisha na kazi ya uzamiaji kwa ajili ya kusafisha eneo la tukio kwa kina cha mita 50 chini ya bahari ili kuepusha ajali zinazoweza kutokea kutokana na meli hiyo na mizigo iliyokuwemo. Kazi hii ilifanyika ili kusafisha njia kwa meli zinazopita katika eneo hilo na kuepusha ajali nyengine kuweza kutokea.

Wakati kazi za uzamiaji zikiendelea, wazamiaji hao walielezea kwamba meli hiyo ilikuwa chini umbali wa kati ya mita 270 mpaka 300. Hivyo, kutokana na vifaa walivyokuwanvyo hakukuwa na uwezekano wa kuifikia, na hata kama ikifikiwa uwezekano wa kukuta watu wakiwa hai haukuwepo tena na miili yao itakuwa katika hali mbaya sana.

Kutokana na hali hiyo, wataalamu hao waliishauri serikali kupitia kamati ya kitaifa ya kukabiliana na maafa kusitisha rasmi zoezi hilo tarehe 16/9/2011.

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais ilituma ujumbe wa watu wawili kwenda Mombasa nchini Kenya kufuatilia taarifa za kuokotwa kwa maiti katika fukwe za bahari ya eneo hilo. Jumla ya maiti watano walipatikana na kuzikwa katika maeneo ya Msambweni (1) Shimoni (2) na Wasili (2) chini ya usimamizi wa Balozi mdogo wa Tanzania aliyeko Mombasa. Gharama zilizotumika kwa utafutaji wa mazishi zilifidiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia ujumbe huo. Ujumbe huo ulifanya mazungumzo na viongozi na wananchi wa maeneo hayo juu ya kuendelea kushirikiana na kutafuta na kutoa taarifa za kupatikana maiti na mizigo ya abiria.

Kukusanya taarifa ya watu waliokuwa hawajaonekana kupitia ofisi ya Masheha na Wilaya

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliziagiza ofisi zote za wilaya na sheha kuorodhesha majina ya watu waliokuwa hawajaonekana na ambao walisadikiwa kuwemo katika meli hiyo na kuziwasilisha orodha hizo kwa Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais ili kufanyiwa uhakiki na kupata orodha sahihi kwa ajili ya matumizi na kumbukumbu za baadae. Hadi kufikia tarehe 9/9/2011 siku ambayo iliwekwa kuwa ni ya mwisho kwa kazi za uodhoreshaji, jumla ya watu 2,764 wameripotiwa hawakuonekana kama wakiwa hai au maiti. Hata hivyo, kwa uhakiki wa awali ilibainika kwamba baadhi ya watu waliorodheshwa zaidi ya mara moja katika maeneo tofauti Unguja na Pemba.

Zaira za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kutoa mkono wa pole

Mhe. Spika, Viongozi Wakuu wa Kitaifa wakifuatana na Mawaziri, Naibu Mawaziri, Wabunge na Wawakilishi, Viongozi wa Dini pamoja na viongozi wengine walifanya ziara za kuzipa pole na kuzifariji familia zilizofiwa na zilizopotelewa na ndugu zao kwa wilaya zote zilizoathirika Unguja na Pemba.

Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alianza kisiwani Pemba tarehe 17 – 20 Septemba, 2011. Katika ziara hiyo alizifariji jumla ya familia 1026 na kila familia ilipatiwa uibani wa shilingi laki moja, baadae alimalizia ziara hiyo kwa wilaya zote za Unguja siku ya tarehe 26/9/2011.

Mhe. Makamo wa Kwanza wa Rais alifanya ziara kama hiyo kisiwani Pemba tarehe 13 na 14 Septemba, 2011 ambapo alizifariji na kuzipatia ubani jumla ya familia 129.

Mhe. Makamo wa Pili wa Rais alizana ziara hiyo Unguja kuanzia tarehe 19 hadi 22 Septemba 2011 na alizifariji jumla ya familia 273, kati ya familia 337 zilizosajiliwa kwa wilaya zote za Unguja na kila familia ilipatiwa ubani wa shilingi 100,000/-. Familia zilizobakia zinaendelea kupatiwa ubani wao kwa utaratibu maalum ulioandaliwa. Kwa ujumla hadi kufikia sasa familia 1,299 zimefarijiwa na kupatiwa ubani.

Mhe. Spika, katika ziara hizo, viongozi wote hao waliwaomba wananchi kuwa na subira juu ya tukio hilo na kwamba serikali itaendelea kuwasaidia na iko pamoja nao. Aidha, walielezea kwamba serikali imeunda tume ya watu kumi kwa ajili ya kuchunguza chanzo cha ajali hiyo na kutoa mapendekezo kwa serikali ambapo walisisitiza kuwa mapendekezo yatakayotolewa na tume hiyo yatafanyiwa kazi sambamba na yale yaliyotolewa na Baraza la Usalama la Taifa.

Tume ya Uchunguzi ya kuzama kwa meli

Mhe. Spika, tarehe 17/9/2011 Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alitangaza rasmi kuundwa kwa tume ya watu 10 ya uchunguzi kwa tukio la kuzama kwa Meli ya *M.V. Spice Islanders.* Tume hiyo inaongozwa na Mwenyekiti wake Jaji wa Mahakama Kuu ya Zanzibar, Mhe. Abdulhakim Ameir Issa na sasa Tume hiyo

imeshaanza kazi zake rasmi. Tume hiyo itatoa ripoti yake serikalini si zaidi ya mwezi mmoja kuanzia sasa.

Kuratibu upokeaji wa misaada

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kitaifa ya Kukabiliana na Maafa inaendelea kupokea misaada ya kifedha na vifaa kutoka kwa watu binafsi, Ofisi za Kibalozi, Mashirika ya Kimataifa, Mashirika ya Umma, Vyama vya Kisiasa, Taasisi za Kidini, Mashirika yasiyo ya Kiserika na taasisi mbali mbali za ndani na nje ya nchi. Hadi kufikia tarehe 11/10/2011 jumla ya shilingi 1,002,775,571/- zimepokelewa na kuingizwa katika akaunti ya Mfuko wa Maafa Zanzibar iliyoko Benki ya Watu wa Zanzibar, ambayo imefunguliwa maalum kwa ajili ya michango hiyo.

Aidha, vifaa na bidhaa mbali mbali zimepokelewa kwa ajili ya kusaidia shughuli za operesheni. Hivi sasa serikali inazingatia kwa makini namna ya fedha hizo zitakavyotumika ili kufikia malengo yaliyokusudiwa. Serikali itajadili na kuamua juu ya namna ya kuzitumia fedha hizo.

Gharama za Operesheni

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliipatia Kamati ya Kitaifa ya Kukabiliana na Maafa jumla ya shilingi milioni mia moja kwa ajili ya kugharamia shughuli za uokoaji ambapo hadi kufikia tarehe 30/9/2011 fedha zilizotumika ni shilingi 99,984,386/-. Matumizi haya hayahusiani na fedha zilizotolewa kwa ajili ya ubani na uendeshaji wa kazi za Tume ya Uchaguzi.

Kwa upande wa kutoa ubani kwa ajili ya familia zilizopatwa na msiba huo, serikali imetoa kiasi ya shilingi 156,000,000/-.

Tulichojifunza kutokana na tukio hili

Mhe. Spika, kutokana na tukio hili la kuzama kwa Meli ya *M.V. Spice Islander*s tumeweza kujifunza mambo mbali mbali, ambayo ni changamoto kwetu katika kuimarisha kazi na huduma za kukabiliana na maafa nchini. Miongoni mwa mambo hayo kwa mtazamo wa Kamati ya Maafa ni haya yafuatayo:-

1. Umakini na maamuzi sahihi na ya haraka yaliyochukuliwa na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi yameweza kuleta ufanisi mkubwa katika uokozi na hivyo kupelekea kuokoa maisha ya wananchi wetu wengi.
2. Pamoja na mazingira magumu ya eneo ilikotokea ajali, muitikio wa haraka wananchi, hasa wa maeneo ya Nungwi na wa taasisi mbalimbali za kukabiliana na maafa, zikiwemo taasisi za serikali, vyombo vya ulinzi na usalama, washirika wa maendeleo, sekta binafsi na jumuiya za kiraia, wamepelekea watu wengi kuweza kuokolewa wakiwa hai, pamoja na

kupatikana kwa maiti hali ambayo imewezesha maiti wengi kuzikwa na familia zao.

3. Ipo haja ya kuimarisha huduma za mawasiliano wakati wa maafa. Hii inatokana na sababu kwamba, wananchi wengi walitumia mtandao wa mawasiliano wa *Zantel* na kusababisha ugumu wa mawasiliano kutokana na minara ya kampuni hiyo kuzidiwa na matumizi.

4. Udogo wa sehemu ya kuhifadhia maiti (*mortuary*) ulipelekea maiti wasiotambuliwa na jamaa zao kuzikwa haraka na serikali.

5. Uhaba wa vifaa vya kisasa vya uokozi pamoja na wataalamu wazamiaji kulipelekea zoezi la uokozi kuwa gumu na kuchukua muda mrefu.

6. Kukosekana kwa taarifa za uwezo wetu wa ndani wa kukabiliana na maafa ikiwemo uwezo wa vifaa na wataalamu ni changamoto ambayo inapaswa kufanyiwa kazi.

7. Kukosekana kwa mkakati madhubuti wa kujikinga na maafa ya majini kivifaa na wataalamu kunapelekea kupata majanga ya ajali za vyombo vya usafiri kwa abiria mara kwa mara.

Mikakati ya Serikali katika kukabiliana na maafa

Mhe. Spika, katika kukabiliana na majanga na maafa mbali mbali yanayoweza kutokea katika nchi yetu, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imedhamiria kutekeleza mikakati mbalimbali ya kukabiliana na maafa ikiwemo hii ifuatayo:-

1. Kuifanyia mapitio sheria nambari 2 ya mwaka 2003 ya kukabiliana na maafa ili iendane na mahitaji na mazingira ya hivi sasa.

2. Kutekeleza kikamilifu mpango wa taifa wa kukabiliana na maafa pamoja na mkakati wa mawasiliano wakati wa maafa.

3. Kujenga uwezo wa kitaasisi katika kukabiliana na maafa ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa vifaa na mafunzo kwa wadau mbalimbali.

4. Kutafuta ushauri wa kitaalamu juu ya kuwa na mbinu madhubuti za kujikinga na majanga na maafa mbalimbali yanayoweza kutokea katika nchi yetu pamoja na kufikiria uwezekano wa kuanzisha vituo vya uokozi katika maeneo mbali mbali ya visiwa vya Unguja na Pemba.

5. Kuendelea kutoa elimu ya kukabiliana na maafa kwa jamii na kuimarisha Kamati ya Maafa za Shehia, Wilaya na Taifa.

6. Kudhibiti utaratibu wa vyombo vya usafiri juu ya abiria na mizigo ya baharini na nchi kavu ili kuepusha ajali na upotevu wa maisha na mali za wananchi.

SHUKURANI

Mhe. Spika, kwa niaba ya Kamati ya Kitaifa ya Kukabiliana na Maafa, naomba nimshukuru sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa juhudi zake kubwa alizochukua ili kuhakikisha maisha ya wananchi yanaokolewa. Tunamshukuru kwa maelekezo yake na miongozo aliyotupatia ambayo kwa kiwango kikubwa ilitusaidia kufanikisha kazi za ukozi.

Tunamshukuru Mhe. Rais Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuwa nasi kwa hali na mali katika kipindi chote cha maafa haya.

Vile vile tunamshukuru Makamo wa Kwanza wa Rais, Mhe. Maalim Seif Sharif Hamad kwa kutupatia miongozo ya mara kwa mara katika jitihada za kuokoa maisha ya wananchi na kupunguza athari za maafa yaliyotokea.

Tunatoa shukurani za dhati kwa Baraza la Mapinduzi na Baraza la Usalama la Taifa kwa maelekezo yao juu ya hatua za kuchukuliwa katika kukabiliana na janga hili na majanga yanayoweza kutokea baadae. Shukurani za dhati pia zinatolea kwa vyombo vya ulinzi na usalama kwa hatua zao za haraka zilizosaidia kuokoa maisha ya wananchi wengi.

Mhe. Spika, shukurani pia zinatolewa kwa wamiliki wa vyombo vya usafiri majini, angani na nchi kavu kwa jinsi walivyoshirikiana na serikali katika kulikabili tukio hili. Wananchi wa Nungwi hasa wavuvi na wamiliki wa hoteli na wa kampuni za kitalii wanapewa shukurani za pekee kwa jinsi walivyoshiriki kikamilifu tokea hatua za awali baada ya kupatikana taarifa za kuzama kwa meli hiyo.

Tunawashukuru washirika wa maendeleo na wawakilishi wa nchi marafiki kwa jinsi walivyochukulia suala hili na kutuunga mkono katika msiba huu mkubwa wa kitaifa. Vile vile tunazishukuru taasisi za kidini hasa Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana na Ofisi ya Mufti kwa kusaidia maandalizi ya mazishi ya marehemu wote waliotokana na ajali hii.

Tunawashukuru madaktari na wauguzi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja, Kivunge na Bububu jeshini kwa namna walivyoshirikiana na kamati. Tunawashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Kitaifa ya Kukabiliana na Maafa na wafanyakazi wa Idara ya Kukabiliana na Maafa kwa kazi kubwa walivyoifanya kwa kipindi chote tokea kutokea kwa janga hili.

Tunawashukuru wamiliki wa vyombo vya habari na wana habrai na wananchi wote wa Zanzibar na Tanzania kwa jumla kwa kupokea tukio hili kwa masikitiko makubwa. Aidha, tunawashukuru wale wote walioweza kuchangia kwa hali na mali katika msiba huu ikiwa pamoja na Baraza lako tukufu Mhe. Spika.

Mwisho kabisa Mhe. Spika, baada ya kutoa maelezo hayo naomba Wajumbe wa Baraza lako tukufu waipokee taarifa hii na kuitafakari.

Mhe. Spika, sasa kwa heshima na taadhima naomba kuwasilisha.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Makamo wa Pili wa Rais, kwa kuwasilisha taarifa hiyo ya serikali ambayo Waheshimiwa Wajumbe wamekuwa wanaisikiliza kwa makini sana, kwa sababu ya uzito na umuhimu wake. Kama ilivyo kawaida kauli huwa haijadiliwi, lakini tunaweza tukauliza maswali na hatimaye kupata ufafanuzi wa maswali hayo. Kwa sababu kama tunavyoelewa katika taarifa hii Mhe. Makamo wa Pili wa Rais ameelezea kwamba kuna tume iliyoundwa ambayo nayo itakuja kutupa taarifa yake baada ya kumaliza uchunguzi. Sasa kabla ya kuwapa nafasi Waheshimiwa Wajumbe kuuliza

maswali basi tumkaribishe Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ovisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa.

Taarifa ya Kamati ya Baraza la Wawakilishi ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa Juu ya Tukio la Kuzama Kwa Meli ya Mv Spice Islanders Iliyotokea Tarehe 10.09.2011 Katika Eneo la Mkondo wa Bahari ya Nungwi, Zanzibar

UTANGULIZI

Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa: (Mhe. Hamza Hassan Juma): Mhe. Spika, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kukutana tena mbele ya Baraza lako tukufu, tukiwa wazima wa afya ili kujadili mambo mbali mbali yanayohusu maendeleo ya nchi yetu.

Mhe. Spika, pia napenda kuchukua fursa hii kuishukuru Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuwasilisha taarifa inayohusiana na tukio la kuzama kwa meli ya Mv Spice Islanders I iliyotokea katika mkondo wa bahari ya Nungwi, Zanzibar, mnamo tarehe 10.09.2011. Ni mwezi mmoja hivi sasa, lakini bado tunakumbuka tukio hilo la kihistoria ambalo hatutoweza kulisahau maishani mwetu Wazanzibari sote.

Mhe. Spika, ndugu zetu waliopoteza jamaa zao na pia wale walionusurika katika ajali hiyo tunawatakia afya njema na pia waliopata matatizo ya mshtuko kutokana na tukio hilo na hasa kiafya, tunawaombea kwa Mwenyezi Mungu awape afueni ili tuweze kujumuika nao katika kuweza kuendelea na majukumu yetu ya kujenga taifa letu.

Mhe. Spika, Aidha kwa niaba ya kamati nakushukuru wewe binafsi kwa kuniruhusu kusimama mbele ya Baraza lako tukufu ili niwasilishe taarifa ya kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa juu ya tukio hilo la maafa.

Mhe. Spika, kwa niaba ya kamati, nachukua fursa hii kumuomba Mwenyezi Mungu awalaze mahali pema peponi wale wote waliofariki kutokana na ajali hiyo, na pia kuwataka kuwa na subira wale wote waliopoteza ndugu na jamaa zao. Pia wale walionusurika katika ajali hiyo na kuwatakia afya njema na pia waliopata matatizo ya mshituko kutokana na tukiou kiafya tunawaombea Mwenyezi Mungu awape afueni ili tuweze kujumuika nao na kuweza kuendelea na majukumu ya kujenga Taifa letu.

Mhe. Spika, Sisi Wajumbe wako wa Baraza la Wawakilishi pamoja na wewe mwenyewe binafsi tulipata mshtuko mkubwa usiku wa manane wa kuamkia tarehe 10.9.2011 wakati tuko safarini kikazi huko mjini Arusha. Baada ya kupokea simu kutoka kwa watu mbali mbali kuhusu tukio hilo kubwa la aina yake kwa hapa Zanzibar kwa kweli hakuna aliyeamini taarifa hizo na tulianza kupiga simu huku Zanzibar kwa watu tofauti ili kupata uthibitisho wa tukio hilo.

Baada ya kupata uthibitisho wa ajali hiyo tulipigiana simu katika mahoteli mbali mbali tuliofikia ukiwemo wewe mwenyewe ili kujuulishana yaliyotokea Zanzibar na baadae kwa busara zako ukaamua tuahirishe safari na turudi Unguja alfajiri hiyo hiyo.

Mhe. Spika, Baada ya Waheshimiwa Wajumbe kuanza kupata taarifa Kwenye mahoteli tofauti tuliofikia vilio vilitawala kwenye mahoteli yetu na hata aliyekuwa sagu machozi yalimtoka, waliorudi kwa mabasi vilio vilitawala kutoka Arusha hadi Dar es Salam kwani kila mmoja alikuwa na fikra tofauti hajui nani alikuemo kwenye meli hiyo ama ndugu, jamaa au rafiki. Mhe. Spika, sisi wengine nikiwemo mimi mwenyewe binafsi pia nilipata simu kutoka kwa ndugu zangu kwamba ndani ya meli hiyo alikuwemo mtoto wa shangazi yangu yeye pamoja na watoto wake watatu walikuwemo katika meli hiyo wakitokea Unguja kurudi nyumbani kwao Pemba. Hadi leo Mhe. Spika, nasimama mbele ya Baraza lako tukufu hatukuweza kuwaona aidha wako hai au maiti.

Mhe. Spika, isitoshe kutokana na ukubwa wa ajali hiyo hata kama mtu hakuna ndugu au jamaa yako basi lazima machozi yangemtoka, kutokana na kuwafikiria ni hali gani iliyokuwemo kwenye meli hiyo wakati kila mmoja aliyekuwemo alikuwa akiona hivi hivi kuwa wakati wake wa kuaga dunia umefika.

Mhe. Spika, kifo si kitu cha mchezo hata kidogo na wala sio kitu cha masihara na ndio mana hata Mwenyezi Mungu akakiekea pazia, akakifanya kuwa ni siri yake peke yake, hakutoa nafuu kwa mtu yeyote kujua ni lini au wakati gani ataaga dunia. Alifanya hivyo kwa makusudi, kwani kwa binaadamu yeyote kama angelikuwa anashauriwa kufa basi hakuna angelikubali, hata kama tajiri basi angelikubali kutoa mali yake yote ili abaki hai hapa duniani.

Je Mhe. Spika, hebu tufumbe macho na tuvute fikra, je tuone wakati meli inazama wenzetu walikuwa katika hali gani. Kwani wao walipata bahati ya kushuhudia vifo vyao. Mhe. Spika, tuwafikirie wanawake waliokuwa na watoto wao ndani ya meli hiyo walikuwa katika hali gani, tuwafikirie waliokuwa na wake zao ndani ya meli hiyo walikuwa na hali gani, tuwafirie waliokuwa na wazee wao ndani ya meli hiyo walikuwa katika hali gani. Halikadhalika waliokuwa na ndugu, jamaa na marafiki waliokuwa wamefuatana pamoja ndani ya meli hiyo walikuwa katika hali gani.

Mhe. Spika, bilashaka fadhaa ilikuwa kubwa ndani ya meli hiyo kwani hakuna ambaye angelikuwa na uwezo wa kuokoa maisha ya mwenziwe isipokuwa Allah (S.W). Mhe. Spika, kwa taarifa, meli haikuzama ghafla ilianza kujaa maji kwa upande wa nyuma katika mkondo mkubwa Nungwi wenye kina kirefu cha maji na mawimbi makali, ambapo wakati wote meli hata ikiwa na ukubwa kiasi gani basi hupata tabu kupita katika eneo hilo.

Mhe. Spika, usiku huo wa manane wakati wengi wa abiria hao walikuwa wamelala ghafla waliamshwa na mawimbi ya maji yaliyoanza kuingia ndani ya meli hiyo, pamoja na vilio vya wenzao na wao wakapata mfadhaiko na kushuhudia waliokuwemo ndani ya meli hiyo ikianza kuzama na kushuhudia kwa macho yao kwamba ndio mwisho wao wa kuaga dunia.

Mhe. Spika, hebu tufikirie mfano humu ndani ya ukumbi wa Baraza, kama ingekuwa ndio meli hiyo na sisi ndo abiria je hapa hali ingekuaje.

Mhe. Spika, hili ni tukio la kweli na wala si mchezo wa kuigiza, huu ni msiba mkubwa wa kitaifa na hatuwezi kuusahau milele, tukitaka tusitake vifo walivyokufa wenzetu ni vibaya sana, ingawa ni uwezo wa Mwenyezi Mungu lakini ukweli vifo hivyo viliuma sana.

Mhe. Spika, sisi tukiwa Wawakilishi wa Wananchi tunaitaka Serikali ichukue hatua kali sana za kinidhamu kutokana na uzembe mkubwa uliosababisha ajali hiyo ambayo haiwezi kusahaulika na ambayo imepoteza roho nyingi za ndugu zetu pamoja na mali zao.

Mhe. Spika, kamati yangu baada ya kupokea taarifa kutoka kwa Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais juu ya tukio la kuzama kwa meli ya Mv Spice Islanders jana imekutana na kujadili kwa kina na kuja na maoni yafuatayo kuhusiana na taarifa hiyo.

Mhe. Spika, kwanza ripoti imeeleza kuwa meli hiyo imesajiliwa kubeba abiria 610 ambapo ikiwa itatokea ajali ingekuwa na *life jacket* 610 na ingekuwa wepesi wa kuokolewa kutokana na vifaa vilivyopaswa kuwemo kwenye meli hiyo. Lakini uhalisia meli hiyo ilipakia abiria wengi sana zaidi ya 2,764 mara tano ya uwezo wa meli hiyo. Hii inadhihirisha **uzembe wa makusudi** uliofanywa na wahusika mbali mbali wanaohudumia na kusimamia idadi na usalama wa abiria wanapo safiri kwenye meli.

Mhe Spika ndani ya Baraza lako tukufu tumekuwa tukipiga kelele siku zote namna ya udhibiti wa idadi ya uingiaji wa watu melini, Waziri amekuwa akitoa jawabu za kubahatisha asizokuwa na uhakika nazo, pia kudharau na kutokujali taarifa mbali mbali zinazotolewa na wananchi kupitia vyombo mbali mbali vya habari, yakiwemo magazeti na redio, na matokeo yake ndio kama hayo.

Kwa mfano Mhe. Spika, **TAARIFA YA WAZIRI WA MIUNDOMBINU NA MAWASILIANO JUU YA HITILAFU KWA VYOMBO VYA BAHARINI SIKU ZA HIVI KARIBUNI:**

Mhe Spika naomba kunukuu baadhi ya maneno yake kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, “Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano, kupitia mamlaka yake ya usafiri baharini imekuwa ikipokea taarifa mbali mbali kuhusiana na usafiri na mwenendo mzima wa vyombo vya Baharini; anaendelea. Taarifa hizi zimekuwa zikifuatiliwa na wizara yangu kupitia redio, magazeti n.k. Hata hivyo, wizara yangu imekuwa ikizifuatilia kwa karibu na kujitahidi kuzihakiki na kugundua nyingi ya taarifa hizo zinazotolewa zinautata, kwa hivyo inapelekea kuleta tafsiri nyingine kwa jamii, tafsiri zinazoleta taharuki kwa jamii.” Mwisho wa kunukuu.

Mhe Spika pia waziri huyo akalidanganya Baraza lako tukufu kwa kusema naomba kunukuu tena.

Mhe Spika, waziri anasema, “Mhe. Spika, naomba kutoa pole kwa wale wote waliopata athari na usumbufu kutokana na taarifa hizo zilizokuwa zimeleta utata. Aidha, nalihakikishia Baraza lako tukufu na wananchi wote wa Zanzibar wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kupitia malaka ya usafiri baharini wanachukua hatua zote za kiusalama kwa vyombo vya baharini kabla ya vyombo kuondoka na kufanya safari zake.

Aidha, tutaendelea kuchukua hatua zote za kiusalama kwa vyombo vyote vinavyofanya safari hizo, kufanya huduma hizo za kusafirisha abiria ikiwemo kuvikagua na kuvithibitisha juu ya safari zake hizo kabla ya kuondoka”.
Mwisho wa kunukuu, Je Mhe. Spika, katika meli hiyo haya maneno ya waziri aliyotuambia hapa Barazani yalifanyika?.

Ndio maana kamati yangu ikabaini kwamba kunaubabaishaji mkubwa wa kiutendaji katika wizara hii na kukaa ofisini na kutuletea taarifa za kujifurahisha wao na sio za uhalisia.

Mhe Spika, kutokana na uzembe huo uliofanywa na wizara imeonyesha wazi wazi kuwa Waziri wa Mawasiliano na Miundombinu, ameshindwa kusimamia ipasavyo majukumu yake aliyopewa na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, na kwa kuwa kwa mujibu wa Sheria na *Regulation* zinazoongoza mamlaka ya usafiri wa baharini, kuna kipengele kinachomtaka Waziri kuunda tume linapotokea jambo kama hilo, lakini kwa busara Mhe. Rais ameamua kuchukua jukumu yeye mwenyewe la kuunda tume. Hii ni wazi ameona waziri naye amehusika katika ajali hiyo, ndio maana maana hakumsubiri kuunda tume yake.

Mhe. Spika, kwa maana hiyo hapa tunamtaka Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano **ajiuzulu** kwa hiari yake, ili kuonyesha uwajibikaji na asisubiri kuwajibishwa na Mhe. Rais kwa uzembe wa kutokusimamia majukumu aliyopewa na serikali. Tunaamini akifanya hivyo, itakuwa ni kweli serikali yetu inawajibika kwa wananchi na hata Mwenyezi Mungu amesema, kwamba kila mchunga ataulizwa kwa kile alichokichunga. Hiyo ndio Demokrasia na utawala bora unavyotaka, kwani Demokrasia Mhe. Spika, ni gharama. Tusione taabu kuwajibika pale inapobidi, hasa kutokana na uzito wa jambo lenyewe.

Mhe Spika, kama kweli tunataka tuendelee lazima tubadilike kama anavyosema Mhe. Rais wetu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwamba *BUSSINESS AS USSUAL* yaani tusifanye kazi kama tulivyozoea, tubadilike ili tufike kule tunakotaka kwenda.

Mhe. Spika, kuna mifano mingi ya serikali kuwajibika duniani tangu kuchaguliwa Rais mwanamke wa Brazil Bi Roshelina, kuanzia mwezi Januari mwaka huu wa 2011 hadi sasa karibu mawaziri wanne wamejiuzulu kwa hiari yao, kutokana na makosa mbali

mbali ya taasisi zao. Ikiwemo Japan ndani ya miaka mitano karibu mawaziri wakuu sita wamejizulu kutokana na kuwajibika kutokana na uzembe katika taasisi zao.

Kwa hapa Tanzania Rais mstaafu wa Zanzibar na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mzee wetu Ali Hassan Mwinyi, alijiuzulu kutokana na vifo vya wafungwa gerezani alipokuwa Waziri wa Mambo ya ndani na sio mkuu wa Magereza aliyewajibika, wakati wa utawala wa Mwalim Nyerere. Kwa hivyo, hilo sio jambo geni hata kwa Tanzania, bado kuna haja ya serikali yetu kuonyesha uwajibikaji kwa wananchi wake.

Mhe Spika, bado kamati yangu imeona kulitokea uzembe mkubwa kutoka kwa kepteni wa meli hiyo kwa kushindwa kutoa taarifa mapema, wakati meli ilipoanza kuingia maji hadi hapo abiria wenyewe walipoanza kupiga simu wakiwa juu ya meli. Tunaamini kwamba kepteni angelitoa taarifa mapema, basi abiria wengi sana wangeliokolewa wakiwa hai. Nadhani kwa kuwa ulikuwa usiku wangelipiga fataki kurusha angani ingelisaidia kujulisha waokoaji kujua chombo kiko mahala gani, kwani abiria walikaa baharini karibu masaa 5 wakiwa hawajapata msaada wa aina yoyote, wakati tukio limetokea pahala ambapo panafikika kwa ndani ya nusu saa au saa moja tu. Tunaamini waokozi wangelifika mapema hali isingekuwa ya maafa makubwa kiasi kama hicho.

Mhe. Spika, kamati inashauri meli zote ziwe na fataki za kupiga angani pindipo ikitokea janga kama hilo, kwani wakati wowote majanga kama hayo huweza kutokea.

Mhe Spika, suala la uzembe wa kutojua idadi ya abiria waliopanda kwenye chombo umekuwa ni kitu cha kawaida, kwa wenye vyombo na watendaji wa serikali wanashuhudia pale meli zinapoondoka, hakuna anayejali.

Kwa mfano, baada ya kuzama meli ya MV. FATIH waziri aliahidi kuwa sasa mtu yeyote anayetaka kusafiri nje ya Zanzibar ni lazima aende na kitambulisho. Je hilo linafanyika? Au wajumbe wako huwa wanaondolewa njiani tu wakati wa vikao vya Baraza? Kama suala hilo lingesimamiwa basi tayari watu wote waliokuwemo ndani ya meli hiyo wangelikwisha julikana. Lakini kutokana na uzembe huo hakuna kinachofanyika, hii inaonyesha ni namna gani baadhi ya viongozi wanavyoshindwa kusimamia majukumu yao, pia kutojua thamani ya raia wetu na wakifa bado watu wengi uchungu hawana.

Mhe Spika kamati yangu haijaridhika na sehemu ya taarifa ya serikali inayosema, kwamba kuna majina yaliyopelekwa mara mbili. Sisi tunaamini kwa kushirikiana na Wakuu wa Mikoa, majina yanaweza kukusanywa na yakaangaliwa yote kwa pamoja na kuangalia yaliyofanana na kufuatiliwa taarifa zake na marekebisho yakafanywa haraka. Mhe. Spika, ni aibu katika karne hii ya 21 tunashindwa kulinganisha vitu kama hivi vya majina yaliyofanana hasa kwa taarifa ya msiba kama huu mkubwa uliotokea.

Mhe Spika, pia kamati yangu haikuridhika na taarifa ilyotolewa na serikali kuhusu kushindwa kazi kwa wazamiaji kutoka Afrika ya Kusini, eti kwa sababu ya kina kirefu cha maji. Kwani hapo mwanzo walipoitwa kwani hawakupewa taarifa kamili kuhusu eneo la tukio na kima cha maji kilichopo? Kwani tulipata taarifa za awali kutoka kwa wazamiaji wetu wa hapa Zanzibar kwamba wamejaribu kuzamia na walifika zaidi ya

mita 100 na wakagundua kwamba kina cha maji cha hapo Nungwi kilikuwa ni zaidi ya mita 300, kabla ya kuja hao ndugu zetu kutoka Afrika ya Kusini. Kwa hivyo, tunaitaka serikali tujifunze kutokana na makosa yetu, wakati na siku yoyote tutakapohitaji msaada kutoka kwa wenzetu au kwa nchi jirani basi tuwape taarifa za kutosha kwa kazi watakayokuja kuifanya, ili na wao kuweza kujitayarisha na vifaa na zana zinazostahili, kama uwezo wao utakuwa ni mdogo basi waweze kutujuulisha mapema. Lakini pamoja na kasoro hizo za kiutendaji tunawashukuru sana ndugu zetu wa damu kutoka Afrika ya Kusini, tunaamini walikuja kutusaidia, lakini hawakupata taarifa sahihi zilizokamilika. Tunawaomba na mara nyingine tukiwahitaji basi wasisite kuja kutusaidia, ingawa hatuombi maafa mengine yatokee.

Kamati kwa niaba ya wananchi wote wa Zanzibar tunaomba serikali itupelekee pongezi hizo kwa Serikali ya Afrika ya Kusini.

Mhe Spika, pamoja na kuchelewa kufika kwenye tukio kutokana na kutojua chombo mahala kilipokuwepo, lakini tunatoa pongezi zetu za dhati, hasa kwa Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, pamoja na wavuvi na wananchi wa kijiji cha Nungwi bila ya kujali itikadi zao za kisiasa au Dini au jinsia, wakiwemo kinamama waliosadia kuwapokea majeruhi na maiti zilizopokelewa pale katika kituo cha Nungwi. Pia Kikosi cha KMKM kilichotokea Mkoani Pemba, na kuwa wa mwanzo kufika kwenye ajali wakitokea Pemba. Pia Helikopta iliyokuja kugundua na kutoa ishara mahala meli ilipokuwepo.

Vile vile tunawapa pongezi wenye vyombo binafsi yaani *Speed Boat*, pamoja na wawekezaji wa Mahotelini waliotumia *Speed Boat* zao kusaidia kuokoa maiti na majeruhi waliokuwemo kwenye meli hiyo. Kamati yangu inawaomba kuendelea na moyo huo huo wa kusaidiana popote na wakati wowote wakati matukio kama haya yanapotokea na sisi hatuna cha kuwapa isipokuwa Mwenyezi Mungu atawalipa fungu lao kwa kazi kubwa ambayo wameifanya.

Mhe Spika tunaiomba serikali kama tulivyoshauri kwenye ripoti yetu ya kamati kwa Ofisi ya Rais mnamo mwezi wa April mwaka huu wa 2011. Iko haja maalum kwa serikali ya kukiboresha kikosi chetu cha KMKM pamoja na Zimamoto kwa kuvipatia vifaa vya kisasa ili pale yanapotokea maafa basi wawe na uwezo mkubwa wa kukabiliana na maafa hayo.

Mhe. Spika, kwani hivi sasa KMKM wanaukosefu mkubwa wa nguo za kuzamia ukosefu wa chupa za gesi, na chombo cha kumuandaa mzamiaji kabla kwenda kwenye kina kirefu cha maji bila chombo hicho basi kuhatarisha hata usalama wa afya ya muokozi hyo, baya zaidi kwa upande wa Pemba hakuna hata kitengo cha uzamiaji je M.Mungu tena atuepushie mbali ajali ikitokea Pemba basi itabidi waokoaji wachukuliwe kutoka unguja.

Mhe Spika leo hii Pemba kuna *Fibre Boat* za KMKM karibu sita, lakini *engine* iliyoko na moja tu, wakati thamani ya *engine* hizo na shilingi milioni 3 tu kwa kila *engine* moja. Je, hapa kweli tuko *serious* katika kuokoa maisha ya wananchi wetu? Hii ni hatari kubwa na inabidi kamati yangu inashauri serikali kulifanyia kazi mara moja suala hili.

Mhe Spika, kutokana na funzo tulilolipata hivi, ni lazima serikali ifanye jitihada zozote za kununua meli kwa njia yeyote, kama hakuna pesa basi ifunguliwe *account* maalum ya kuomba msaada wa kununuliwa meli, naamini kuna wasamaria wema wengi duniani na wengine wako hapa hapa Zanzibar wataweza kuichangia *account* hiyo ilikuweza kununua meli kwa ajili ya kuokoa maisha ya Wazanzibari. Lakini vile vile kwa ajili ya kuwasafirisha Wazanzibari katika visiwa vya Unguja na Pemba pamoja na Dar es Salaam.

Mhe Spika, kamati yangu inatoa tahadhari nyengine kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwamba yanaweza yakatokea maafa mengine makubwa sana, kama hatua za haraka hazijachukuliwa na serikali ya kuangalia athari itakayokuja kutokea iwapo Hoteli ya *Misali Beach Resort* iliyoko Wesha, ikija kuripuka na kuwaka kama mahoteli mengine yanavyowaka katika maeneo mbali mbali hapa Zanzaibar kutokana na pale ilpo, basi matenki ya maji yaliopo Wesha yataripuka. Pia kama kuna meli inateremsha mafuta itaripuka, na wananchi wanaoishi Wesha watateketea kwa moto. Sasa bora mtu aliepata maafa akafa, kuliko mtu alieungua moto sijui viongozi tutaenda tena kuwafariji watu kwa zamu au tutafanya nini. Kwani hoteli hii imejengwa kiubabe haikufuata taratibu zozote na Idara ya Mazingira ilizuia, Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kusini Pemba alizuia, lakini ilitumika nguvu ya pesa na hoteli hiyo ikajengwa kwa nguvu zote na hivi sasa imekamilika. Likitokea lolote kamati inasema serikali itawajibika.

Mhe Spika, tunashauri serikali, hiyo tume iliyoundwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, ije na taarifa zitakazowaridhisha wananchi. Mfano, kujua wamiliki wa meli, Bima, mwaka ilokaguliwa meli hiyo, vifaa vya uokoaji vilivyokuwemo, ruhusa ya kuondoka bandarini na kusafiri kama kawaida yaani kama sheria ya *maritime authority* inavyoeleza. Hatua kwa wasimamizi waliokuwepo siku ya tukio, na msaada gani kwa familia hasa yatima waliobaki wataweza kushughulikiwa.

Mhe Spika, pia tunatoa pongezi kwa serikali kupitia kamati yake ya maafa, kwa mipango mizuri iliyojipanga na kuweza kuratibu na kuzitambua maiti, majeruhi pamoja na maandalizi ya mazishi kwa wale waliokuwa hawakuonekana na jamaa zao. Pia kutoa huduma ya chakula na usafiri kwa wale waliotaka kurejeshwa makwao.

Halikadhalika tunatoa pongezi kwa madaktari na wahudumu wote wa Hospitali ya Kivunge, Jeshini Bububu na hospitali ya Mnazi Mmoja, kwa kazi kubwa waliyofanya ya kuokoa maisha ya majeruhi waliopelekwa katika hospitali hizo. Tunatoa pongezi za dhati kwa vyombo vyote vya habari kuanzia Redio Nuur walionza kutoa taarifa usiku wa manane, TVZ, Redio Zanzibar, Zanzibar Cable Television na vyombo vyote vya habari vilivyosaidia kuwapasha taarifa wananchi kwa kila tukio lililokuwa likiendelea katika kadhia hiyo ya msiba huo mkubwa.

Mhe Spika pia tunatoa pongezi maalum kwa viongozi wetu wote wa kitaifa, kuanzia Mhe. Rais mwenyewe wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Makamo wake wa Kwanza na wa Makamo wa Pili. Pia Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Makamo wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Waziri Mkuu, Viongozi wa Dini na wananchi mbali mbali pamoja makamanda wa Vikosi vyetu vya

ulinzi na usalama kwa jitihada waliyozionesha kwa mshikamano mkubwa wakaati wote wa tukio hilo na kila mmoja aliwajibika kwa nafasi yake.

Mhe. Spika, kila mmoja kwa nafasi yake katika kutoa msaada uliohitajika, hii inaonesha mshikamano mkubwa kwa nchi yetu hasa kwenye kusaidiana kwenye dhiki na faraja.

Mhe Spika mwisho kabisa tunatoa shukrani kwa wananchi wote wa Zanzibar, kwa mashirikiano waliyotoa wakati wote wa tukio na kutoa msaada wa hali na mali, tunawaomba waendelee kuwa na moyo huo huo wakati wote maafa yanapotokezea.

Mhe. Spika, mwisho kabisa nataka nitowe pongezi maalum kwako wewe mwenyewe Mhe. Makamo wa Pili wa Rais, kwa kuweza kusimamia vizuri majukumu yako ya kusimamia shughuli za serikali.

Mhe. Spika, tulivyokuwa Pemba na Kamati yako ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa, ilikwenda katika eneo la Makangale na ikazuwia ujenzi wa hoteli ya Muyuni Beach Resourt and Bar, ambayo ilikuwa imejengwa kinyume cha taratibu.

Mhe. Spika, pale kulikuwa kuna agizo la serikali, agizo la Idara ya Mazingira kusitisha na kuzuwia ujenzi ule. Mhe. Spika, kama kawaida uongozi wa hoteli ile walipiga simu Zanzibar na baadae mheshimiwa tunashukuru kwamba taarifa hizo ilizipata. Baada ya kuzipata taarifa hizo hukusita. Mhe. Makamo wa Pili wa Rais ulikwenda katika eneo hilo na ulipoona taratibu za kisheria zimekiukwa, ulisimama kidete na msimamo wa kamati na ukaamuru hoteli ile isimamishe ujenzi mpaka hapo itakapopata taratibu za serikali.

Mhe. Spika, kwa msimamo huo Mhe. Makamo wa Pili wa Rais aliouonesha basi kamati yetu inakupongeza sana na iko pamoja na wewe na haitokuwa tayari kumstahamilia na kumvumilia mtu yeyote hata akiwa na pesa kiasi gani, hata kama ana uwezo wa kuinunua Zanzibar nzima, basi kamati yako haitoweza kumstahamilia mtu huyo na kuhakikisha kwamba sheria za nchi zinafuatwa.

Mhe. Spika, baada ya hayo machache naomba kuwasilisha, ahsante. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, hiyo ni ripoti ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa. Wasaa upo kwa ajili ya maswali kutoka kwa Waheshimiwa Wajumbe.

UTARATIBU

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Nakushukuru Mhe. Spika, naomba nianze kwa kukupongeza kwa busara zako ulizozionesha kuruhusu kutumia kanuni ya 153 ili kumuezesha Mhe. Makamo wa Pili wa Rais kuwasilisha kauli hii ya serikali.

Mhe. Spika, kama ulivyotupa muongozo ukihusisha taarifa hii ya serikali na kanuni ya 43, ulituambia kwamba kwa mujibu wa utaratibu huu hapa kinachoruhusiwa ni kuuliza maswali. Tunalitambua hilo Mhe. Spika, lakini nilikuwa nataka kuomba kwamba kwa

busara zote ulizozitumia katika kuitumia kanuni ya 153 kumruhusu Mhe. Makamo wa Pili wa Rais kuwasilisha taarifa hii, basi utumie busara ili kukidhi lile ombi alilokuja nalo Mhe. Makamo wa Pili wa Rais.

Mhe. Spika, katika hotuba yake hii mwisho kabisa Mhe. Makamo wa Pili wa Rais naomba nimnukuu anasema;

> "Mhe. Spika, baada ya kutoa maelezo hayo nawaomba Wajumbe wa Baraza lako tukufu, waipokee, waijadili taarifa hii na kutupatia ushauri ili uweze kutusaidia katika harakati za kukabiliana na maafa hapa nchini"

Mhe. Spika, kwa kawaida kwenye hitimisho ndiko kunakowekwa msingi hasa wa madhumuni ya kile ambacho kimewasilishwa na kwa msingi huo na kwa uzito wa suala hili, pamoja na kutolewa maelezo Mhe. Spika, ambayo nayaheshimu sana kwamba sasa hivi imeundiwa tume, lakini kanuni zetu zinatukataza kuzungumza jambo ambalo liko mahakamani. Suala hili kwa bahati nzuri hata kesi mahakamani imesimamishwa.

Kwa hivyo, sidhani kama Baraza lako litakuwa linatenda kosa ikiwa utaturuhusu wajumbe wako kujadili taarifa hizo alizowasilisha Mhe. Makamo wa Pili wa Rais na hasa kutokana na kuwa imewasilishwa. Kwa hivyo, suala la kukiuka kanuni litakuwa halipo tena. Tunaomba hii kanuni inayozungumzia kuuliza maswali tu kwa kauli za mawaziri itengwe kando kwa muongozo wako Mhe. Spika, ili kuturuhusu wajumbe wako kujadili suala hili muhimu, nyeti na linalogusa kila roho ya Mzanzibar. Nchi nzima hivi sasa Mhe. Spika, inatuangalia ili kutuona tutafanya nini katika suala hili. Naomba muongozo wako Mhe. Spika, ahsante sana. *(Makofi).*

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Spika, kwanza naomba nikushukuru kwa kunipa fursa hii. Pili naomba nimshukuru Mhe. Ismail Jussa Ladhu naamini ombi lake lilikuwa na nia nzuri ya kuliwezesha Baraza kujadili suala hili linalohusiana na taarifa hii kwa madhumuni ya kuleta ufanisi katika utendaji wa serikali.

Mhe. Spika, kwanza nitangulie kusema kwamba labda hii taarifa iliyosambazwa kwa wajumbe na taarifa ambayo Mhe. Makamo wa Pili wa Rais aliitowa au aliieleza hapa ambayo nadhani ndio iko kwenye Hansard, neno lililotumika ni;

> "Wajumbe wa Baraza lako tukufu waipokee taarifa hii na kuitafakari".
> Hakuna neno kuijadili. Kwa hivyo, hilo ni la kwanza.

La pili nitowa taarifa kwa faida ya Baraza hili kwamba hii kesi haijaondolewa mahakamani, kesi ya kuhusu suala hili imesimamishwa kusikilizwa. Naamini Mhe. Ismail Jussa atakubaliana na mimi kwamba *with drawel* ya kesi ni tofauti na *stay*, yaani hii kesi kuwa *stay* haina maana kwamba haiko mahakamani.

La tatu Mhe. Spika, naomba sana tuzingatie kwamba tume tuliyoipa au Mhe. Rais aliyoipa kufanya kazi hii ni tume ambayo baadae inatakiwa ije na ukiangalie zile *times of reference*, yaani inatakiwa ije na maelekezo kuhusiana na mambo mengi ambayo

yameelezwa katika suala hili. Nadhani madhumuni ya hii taarifa ilikuwa ni kuwezesha kujua kilichotokea na kuwezesha kujua kilichotokea pamoja na hatua zilichochukuliwa, ili wakati uchunguzi unaendelea basi wananchi wajue kwamba hatua, kwa sababu maneno mengi yamesemwa kuhusiana na mambo mbali mbali.

Kwa mfano, hata misaada iliyotolewa wengine wanadhani imekwenda kwa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais mwenyewe na mwaka huu atafaidi sana kwa kupokea ile misaada. Sasa nafikiri hii ilikuwa ni busara ya kuwawezesha wananchi kupata taarifa. Kwa hivyo, ni vyema tutumie busara Mhe. Spika na pia nategemea muongozo wako utatupa busara kwa kuzingatia haya ambayo nimeeleza.

Nakushukuru Mhe. Spika. *(Makofi)*

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, nimesikiliza maelezo ya swahibu yangu Mhe. Mwanasheria Mkuu na mimi naamini kwamba na yeye anayo nia kwa sababu ya uadilifu alionao, kulisaidia Baraza lako liweze kufanya kile ambacho wananchi wa Zanzibar wanakitegemea katika Baraza hili ambalo ni muhimu sana.

Mhe. Spika, nakubali maelezo yake aliyoyasema kwamba kesi iliyokuwepo haikuwa *withdraw* na ninaomba Mhe. Spika, nirejee Kanuni zetu za Baraza kwenye kanuni ya 58 (4) naomba kunukuu.

> Kanuni za Baraza kifungu cha 58 (4) kinasema hivi:-
>
> > “Ni marufuku kwa Mjumbe yeyote kusema jambo lolote linalongojea uamuzi wowote wa Mahakama pamoja na mambo mengine …”

Interest yangu ipo hapa. Mhe. Spika, ikiwa ushauri wa Mhe. Mwanasheria Mkuu kwetu ni sahihi, basi napata matatizo kidogo, kwa sababu kama ni hivyo najiuliza kwa nini serikali ikaleta taarifa hii.

Kwa kweli kama suala hili na uchunguzi wake kwa jumla hatujui sisi kama Wajumbe pamoja na wananchi kwa jumla hatujui nini hadudi za rejea walizopewa tume hii, kwa hiyo hatujui mpaka leo wanachunguza nini?

Sasa pengine katika maelezo haya ambayo serikali imekuja kuyatolea taarifa leo tena kupitia kwa mtu mzito sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, pengine tayari imegusa mambo ambayo yanachunguzwa na labda yako mengine yatakuwa yanagusa yale mambo ambayo yako mahakamani.

Kwa hivyo, nasema kama suala hili tayari limeletwa na serikali kwa ajili ya kujadiliwa hapa, basi naamini serikali kwa ushauri mzuri wa Mhe. Mwanasheria Mkuu wetu pamoja na uwezo wake, ilijua kwa taarifa hii haifanyi makosa wala haivunji Kanuni pamoja na taratibu zetu.

Kwa msingi huo Mhe. Spika, naomba tuijadili taarifa hii na wala hatuijadili nyengine, isipokuwa tuijadili taarifa hii ambayo serikali imetuletea, kwa sababu kama suala hili tunadhani lingekuwa linakiuka Kanuni, basi sifikirii serikali yenyewe chini ya ushauri ya wanasheria wazito tuliokuwa nao ingeleta kitu ambacho inajua kwamba baadaye kitapelekea Baraza hili lionekane linakiuka utaratibu wa utawala wa sheria katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naomba tena utumie utumie umahiri, umakini, busara pamoja hekima zako, ili Baraza lako lisionekane kioja mbele ya wananchi wa Zanzibar. Ahsante sana Mhe. Spika. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, naomba nielezee mambo yanayofuata. Mhe. Mjumbe alitaka kujua ile *rational* ya kusema kwamba Kauli za Mawaziri au Serikali zisijadiliwe. Kwa kweli hii si kwa suala hili tu, isipokuwa ndio utaratibu ulivyo katika mahala mote.

Lakini Mhe. Spika, hii kesi ina maeneo mawili, kwanza kesi bado iko mahakamani na kesi ikiwa mahakamani Mhe. Spika wewe ni mwanasheria unajua hatuwezi kuizungumza na wala haijaondolewa. Vile vile Mhe. Mjumbe anajua tofauti ya *stay of the case and withdrawal of the case*, sasa kesi hii haijawa *withdraw*.

Kwa hivyo, tukijadili chochote hapa mahakama inapotaka kusikiliza kesi hii basi itakuwa tumeshafanya kitu kinachoitwa *prejudice* ambacho hakitakiwi kisheria. Hilo la kwanza.
Mhe. Spika, pili kuhusu hizi *terms of reference* ambazo alizizungumza au alizitanga Mhe. Rais, yaani alizitanga kwenye redio, televisheni pamoja na magazeti na zinajulikana.

Lakini sasa tunapozungumza kitu ambacho tume umeshaundwa na hii tume wanaita ambapo Mhe. Mjumbe anajua ni *quasi judiciary*, yaani inazungumzia mambo yote ya kisheria na iko katika utaratibu huo wa sheria na ndio maana Mwenyekiti wake akawa ni Jaji wa Mahakama Kuu.

Sasa kama kitu hiki hi *quasi judiciary* ambacho kinazungumzwa Mwenyekiti ni Jaji wa Mahakama Kuu na halafu Baraza linazungumza na kutoa maoni yake basi hiyo pia itakuwa haifai kisheria tutawa-*prejudice* hao ambao wameundiwa tume.

Kwa hivyo, Mhe. Spika nadhani na ninapenda nilishauri Baraza lako kwamba utaratibu huu wa kutokuijadili taarifa hii bado uendelee kwa sababu hizo mbili ambazo nimezieleza. Kwa kweli tutakwenda kinyume na utaratibu na hivyo vyombo ambavyo vimeshaundwa kwa ajili ya kufanya masuala haya itakuwa tumeshaanza kuvishavishi kuwa waelekee mwelekeo fulani na hilo ni kosa kwa Baraza hili.

Mhe. Spika, naomba kutoa taarifa hiyo.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, utaratibu upi maana kuna maelezo yametolewa na Mhe. Ismail Jussa Ladhu, Mhe. Mwanasheria Mkuu amezungumza, nilitaka kusimama lakini Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria alikuwa na maelezo sasa kuhusu utaratibu juu na nini?

UTARATIBU

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, kwa kuzingatia maelezo ya Mhe. Ismail Jussa Ladhu, Mhe. Mwanasheria Mkuu pamoja na Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria serikali imekiri kwamba jambo hili bado lipo mahakamani. Kwa hivyo, niwaombe Waheshimiwa Wawakilishi wenzangu kupitia kwako hata maswali tusiulize tuiachie serikali. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, unajua unapokuwa na jambo kubwa kama hili tunapaswa kuchukua busara zote.

Nakushukuruni Waheshimiwa Wajumbe kwamba nia yetu sote humu ndani ni aina moja, tunakubali kuwa jambo hili ni zito kama vile ambavyo imeelezwa kabla tangu lilipotokea jambo lenyewe, serikali ikachukua hatua, vyombo vikuu vya nchi hii vikachukua hatua. Kwa upande wa vyombo vikuu vya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya Baraza la Taifa la Usalama pia navyo vikachukua hatua kwa sababu ya ukubwa wa jambo lenyewe.

Kwa hivyo, hili halina ubishi kuwa jambo hili ni kubwa na sote naamini kabisa kwamba tunaona uzito pamoja na umuhimu wa jambo hili na maisha ya watu waliopotea. Sasa katika hili naamini hakuna jambo la kupingana, isipokuwa nataka nishauri suala moja kwamba unapojadili jambo katika chombo kama hiki, maana yake hatimaye unataka ufanye maamuzi na huo ndio utaratibu na hilo tunaweza kuamua, lakini hatimaye ufanye maamuzi.

Waheshimiwa Wajumbe, kama mtakumbuka tulikuwa na taarifa ya aina kama hii kuhusiana na suala la mafuta, yaani ilikuja kama taarifa Kauli ya Waziri, lakini ikawa inatakiwa ijadiliwe.
Kwa hivyo, ikabidi taarifa ile badala ya kuja kama Kauli ya Waziri sasa iwe kama ni Hoja ya Serikali, ambayo ilitaka mchango, mtazamo pamoja na uamuzi wa Baraza juu ya kuishauri serikali kuhusiana na suala lile na tulifanya hivyo. Kwa kweli tulifanya maamuzi yetu sisi kama Baraza kuiambia serikali, hivyo serikali inachukua hatua juu ya jambo lile.

Lakini suala hili bado kuna mambo mengi ambayo hayajafafanuliwa. Waheshimiwa Wajumbe, tungeweza kusema kwamba basi Baraza hili liunde tume, tungesema tuunde tume hapa maana yake tukachunguze, lakini tukaona kazi hiyo haina haja, kwa sababu kuna tume ya serikali ambayo imeundwa na inakuwa na watalaamu ambao watachunguza jambo hili.

Kwa nini ikaundwa tume? Sababu za kuundwa tume na serikali ni kama vile ambavyo na kama isingekuwa hivyo basi sisi tungeamua iundwe tume maana yake ifuatilie suala hili kwa kufanywa utafiti pamoja na uchunguzi, ili hatimaye tupate ripoti ambayo tunaweza kuijadili sisi baadaye.

Sasa mambo yote hayo mawili madhumuni pamoja na mtazamo wake ni kwamba jambo hili bado halijapata ufafanuzi wa kutosha. Kwa maana hiyo, tukijadili hapa tutakuja

kuamua nini juu ya jambo ambalo hatujapata ufafanuzi wa kutosha na hilo ndilo swali linalokuja kuhusu jambo hili kama tulijadili au tusilijadili, kwa sababu tukijadili maana yake tutoe maamuzi. Kwa hiyo, tunaoa maamuzi gani juu ya jambo ambalo halijapata ufafanuzi wa kutosha.

Waheshimiwa Wajumbe, sawa Mhe. Hija Hassan Hija yeye anasema hata maswali tusiulize. Kwa kweli jambo hilo liko katika mamlaka ya Spika, kwa sababu hata ile kuuliza maswali ni Mamlaka ya Spika, yaani kwa idhini ya Spika ukiangalia Kanunu ya 43, ndio unaweza kutoa fursa ya Waheshimiwa Wajumbe waulize maswali. *(Makofi)*

Mtazamo wa makofi ninayoyaona ya pande zote mbili, yaani serikali pamoja na Waheshimiwa Wajumbe waliowengi kwamba suala hili tunakubaliana na Mhe. Hija Hassan Hija tusiulize maswali. Kutokana na hali hiyo, mnamshauri Spika kwa kutumia Kanuni ile ya 43 kuwa ile idhini ya kuuliza maswali asitoe na hivyo ndivyo inavyoeleza. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, sasa nadhani niiangalie ile *mood* inasemaje, kwa sababu huu upande mmoja wamepiga makofi sana. *(Kicheko/Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, kwa kuwa maswali ambayo yanaweza kuuliza yatakuwa yanatupeleka kule juu ya jambo ambalo halina ufafanuzi, basi nakubali ushauri uliotolewa kwamba tusiulize maswali. Suala la msingi ni kuwa tuipokee taarifa hii ya awali, ili hatimaye tungoje taarifa kamili ya uchunguzi ambapo hapo tutaamua kuja kuijadili au vyenginevyo.

UTARATIBU

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, kwanza nikushukuru tena kwa hekima zako pamoja na muongozo ambao umetupa hivi punde.

Mhe. Spika, hoja iliyotolewa na serikali baada ya kutuletea wenyewe taarifa hii ni kwamba suala hili lita-*prejudice* uchunguzi unaofanyika. Kwa kweli baadhi ya mambo yaliyomo kwenye taarifa hii ni *subject* ya mambo ambayo yanaendelea kuulizwa hayo uliyosema Mhe. Spika mwenyewe kwamba bado hayajapata majibu pamoja na ufafanuzi wa kutosha.

Kwa hivyo, tukiipokea ripoti hii Waheshimiwa Wajumbe wako tutakuwa tumeyakubali yaliomo humu ndani, sasa kesho na kesho kutwa hatutaweza kuja kuyauliza kwa sababu tuliipokea ripoti hii na *hansard* itakuja kutufunga. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naomba tuchukulie kwamba taarifa hii imetolewa na tumeisikia na majibu yatakuja baada ya kupata ripoti ya tume na kuletwa katika Baraza hili na Wajumbe kupata nafasi ya kutosha ya kujadili na kuona upi ukweli na uongo kuhusiana na suala zima hili. Mhe. Spika, nakuomba sana. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, napenda nimfahamishe Mhe. Mjumbe kwamba kupokea katika *terms* za Baraza ni kuwa ile ripoti ambayo imeletwa ndio inayokubaliwa kwamba iwepo na wala hiyo haisimamishi baadaye baada taarifa zitakazotolewa kuja kujadiliwa.

Sasa suala la kukubaliwa ni tofauti na suala la kulipokea, kwa sababu hii ripoti imechukuliwa na Baraza imo katika *hansard*, hivyo kama kutakuwa na suala la kujadili huko baadaye basi si jambo jengine. Kutokana na hali hiyo, tusi-*confuse* na suala la kupokea likatafsiriwa kwa maana pana ambayo siyo anayosema Mhe. Mjumbe.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, nataka nikumbushe zaidi kwamba haja ya kuleta taarifa hii tuliionesha kwenye mikutano yetu ya maandalizi. Kwa hivyo, kama tutakumbuka kwenye Kamati ya Uongozi. Mhe. Ismail Jussa Ladhu wakati Mhe. Spika anaposema wengine husikiliza labda nisimame ndio itakuwa wengine wasiseme. *(Kicheko/Makofi)*

Kwa hivyo, kwenye Kamati ya Uongozi tuliona kwamba kupitia chombo hiki rasmi cha Baraza baada ya tukio lile kubwa basi iwe kimya tu hakuna taarifa rasmi na kwenye Kamati ya Uongozi tulidai kitu kama hiki kiwepo. Vile vile tulikubaliana kwamba taarifa itakayoletwa kwa kuwa uchunguzi bado haujamaliza, basi angalau ioneshe mambo yale ambayo yamechukuliwa na serikali baada ya tukio lile mpaka kufikia hapa.

Kwa kweli nadhani ukiangalia taarifa hii ndio mambo ambayo yamo humo, yaani ndio mambo tuliyoyaomba kwenye Kamati ya Uongozi na kazi ya Kamati ya Uongozi ni kushauri shughuli zetu za humu ndani na tumeshauriana hivyo na tulimuomba Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, basi alete taarifa hii chini ya Kauli ya Serikali na amefanya hivyo. Sasa kama hatukuipokea ni sawa na kumwambia pale alipokuwa mlangoni kumwambia basi hiyo kauli yako toka nayo, sasa na huo utakuwa sio utaratibu.

Waheshimiwa Wajumbe, nadhani tukubaliane kwamba taarifa hii ameileta juu ya hatua za awali ambazo serikali imezifanya baada ya tukio lile kubwa la kuzama kwa Meli ya MV. *Spice Islander*. Kwa hivyo, tukubaliane na kama ni hivyo, basi mimi moja kwa moja anamua kuwauliza Waheshimiwa Wajumbe wale wanaokubali kupokea taarifa hii wanyanyue mikono, wanaokataa kupokea taarifa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Waheshimiwa Wajumbe, taarifa imepokelewa na kazi ya uchunguzi iendelee na hatimaye serikali tunaiomba ituletee taarifa nyengine hapo baadaye tunashukuru.

HOJA ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali ya Mwaka 2011

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kabla hamjaondoka kwa dharura mbali mbali nataka niseme kwamba suala la taarifa hii ilikuwa ni jambo kubwa na kwa chombo hiki kuamua mambo mazito ni sehemu ya kazi yake kubwa. Sasa ingetosha tukasema basi tukapumzike.

Lakini tukiangalia kwenye *order paper* hakuna shughuli nyengine baada ya hii, ndio nikaamua nimuite Mhe. Waziri kwa ajili ya kumaliza uporo wetu wa jana, ili baada ya hapo jioni tusirejee katika shughuli zetu na itakuwa kazi hii imemalizika. *(Makofi)*

Kwa hivyo, niwaombe wale wanaotoka nje kwa dharura kwamba shughuli hii haitachukua muda mkubwa, kwa sababu tunataka tufanye maamuzi na ninahitaji *quorum* itimie ili tufanye maamuzi kwa mujibu wa taratibu zetu. Mhe. Waziri endelea.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, naomba kukushukuru kwa jana kunipa nafasi baada ya kukuomba kwamba nije nifanye majumuisho leo. Kwa kweli hiyo ilinisaidia kukutana na wataalamu wangu kwa yale masuala ambayo ni muhimu.

Mhe. Spika, shukurani zangu za dhati ziende kwa Waheshimiwa Wajumbe waliochangia mswada huu ambao nao ni mgumu hasa kwa maana wazungu wanasema ni *abstract*, yaani mambo yake ni ya kijumla na vitu vyengine ni vya kitaalamu. Lakini pamoja na hayo, wamechangia, wametoa maoni pamoja na kukosoa mule mlimostahiki.

Mhe. Spika, waliochangia mswada huu walikuwa ni Waheshimiwa Wajumbe wako wanane naomba niwataje kwa heshima yao.

1. Mhe. Salmin Awadh Salmin;
2. Mhe. Rashid Seif Suleiman;
3. Mhe. Hija Hassan Hija pamoja na kwamba ni mjumbe wa kamati lakini alikuwa na maoni naye;
4. Mhe. Fatma Mbarouk Said;
5. Mhe. Ismail Jussa Ladhu;
6. Mhe. Subeit Khamis Faki;
7. Mhe. Naibu Waziri wa Afya na
8. Mhe. Mwanasheria Mkuu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, mjadala ulikuwa umeelekeza katika mambo manne. Kwa hivyo, kulikuwa na mambo machache ambayo yalihitaji ufafanuzi na mengine yalirudiwa na Waheshimiwa Wajumbe na mengine pengine hayatakuwa na haja kwa sababu ilikuwa ni lugha tu.

Kwa kweli kulikuwa na suala la kurekebisha lugha hasa Mhe. Ismail Jussa Ladhu ambaye ni mtaalamu kidogo wa Lugha ya Kiswahili na Sheria pamoja na Mhe. Rashid Seif Suleiman. Vile vile kulikuwa na maoni ya vifungu kwa ajili ya kurekebishwa, pia kuna baadhi ya Waheshimiwa Wajumbe walikataa baadhi ya maneno ambayo yalikuwa yanabadilisha maana iliyotakiwa pamoja na ushauri.

Sasa nikianza na majibu naomba nimshukuru Kaimu Mwenyekiti wa Kamati ambayo kwa jumla mengi yao yalikuwa tayari ni yale yaliyosambazwa kwenye masahihisho. Mhe. Spika, kuna jambo moja ambalo alilishikilia tena lenye ugumu kwa kusema kwamba matokeo ya uchunguzi yatangazwe.

Kwa kawaida uchunguzi unaofanywa na Mkemia Mkuu huwa ni siri ya yule aliyepeleka *sample* yake na Afisi ya Mkemia Mkuu na wala sio masuala ya kutangaza *public*, maana mara nyengine huwa uchunguzi ule umewekwa kwa dhamiri ya kufikishwa mahakamani kwa ajili ya kutoa ushahidi au kulieleza jambo ambalo linaathiri maisha ya mmoja na mwengine.

Kwa mfano, pale inapokuwa mtoto amebakwa na ukenda kufanya uchunguzi kwa Mkemia Mkuu na halafu ukatangaza redioni, nadhani hiyo ni kashfa na kumdhalilisha anayehusika, kwa hivyo huwa inabaki ni siri.

Kutokana na hali hiyo, tunawaomba Waheshimiwa Wajumbe wakubali uendelee ule utaratibu unaostahiki kwamba uchunguzi unaofanywa unabaki siri isipokuwa kwa wale wahusika.

Mhe. Salmin Awadh Salmin alikuja na maelezo ya kutushukuru na kusema kwamba waraka ama sheria kidogo imechelewa. Lakini namshukuru Mhe. Fatma Mbarouk Said ambaye alisema *Better late than ever*. Kwa hivyo, alinisaidia kumueleza Mhe. Salmin Awadh Salmin kwamba kwa sababu tumeamua kufanya sasa, basi maana yake tatizo hili limekwisha.

Vile vile Mhe. Mjumbe alikuja na maoni kwamba Mwanasheria Mkuu, ambapo maoni haya yalizungumzwa na Mhe. Rashid Seif Suleiman na baadhi ya wengine kwamba hana kinga kwa mujibu wa kazi zake ngumu. Lakini Mhe. Mwanasheria Mkuu alilitolewa ufafanuzi kwamba hata hii kinga inayostahiki kupewa yule anayefanyakazi katika wadhifa fulani nao pia ina viwango vyake pamoja na taratibu zake.

Kwa hivyo, katika level ile bado hakuhitaji kinga kama ile ya Jaji Mkuu ya *security of tenure* na kwamba kifungu 13 cha Sheria kilikuwa bado kinawalinda watu wa Mkemia.

Mhe. Salmin Awadh Salmin alizungumzie kuhusu suala la kupata chombo cha *DNA*, muda mrefu suala hili linazungumzwa ambalo ni la kitaalamu. Mhe. Spika, taarifa niliyonayo pamoja na mashirikiano na Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto kwamba suala hili liko njiani kukamilika kukipata chombo hicho.

Kwa hivyo, tutaweza kukitumia Wizara ya Afya pamoja na Wizara ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto, kwa sababu ya matatizo wanayopata sana katika suala la kudhalilishwa watoto.

Mhe. Spika, bila ya shaka kulikuwa na suala la kwamba hatuna utaalamu. Lakini haliwezi kuchukua muda zaidi ya miezi sita kufanya utaratibu kama tutakuwa na kile chombo,

kwa sababu ni *operation* ambo watu wa *laboratory* pamoja na watu waliosomea mambo hayo ni kufunzwa tu ule utaratibu. Mhe. Spika, kwa taarifa yako mimi ni *Chemistry* kama watanipa nafasi basi naweza kufanya vile vitu.

Kwa hivyo, kama tunakipata kile kitu basi tutaweza kuwafunza watu wetu kwa muda mfupi wa *refresher course* au kuwapeleka katika ile taasisi iliyotupatia na kupata mafunzo.

Kuna suala ambalo hili nahisi lilikwenda *a cross the board* na nadhani ni moja katika hoja muhimu ya kuitolea maelezo ni suala la uamuzi wa mwisho, kwamba mkemia mkuu awe ni muamuzi wa mwisho hili amelitaja Mhe. Salmin Awadh, Mhe. Rashid Seif, na mwengine ambae simkumbuki vizuri vile vile, ikawa ni hoja kwamba asiwe muamuzi wa mwisho. Lakini kwa kawaida taasisi kama hii huwa inafanya shughuli zake kwa kushirikiana na taasisi nyengine hasa zile taasisi ambazo zinafanya shughuli kama hii, kuna lugha ya kitaalam inaitwa *supra national* yaani ni chombo ambacho mnakuwa mnafanya kazi pamoja na kwamba linapokuwa suala hili lina ugumu huwa huko mnafanya *reference.*

Lakini hata katika kipimo hicho bado baada ya kupata usahihi inarudi kwamba Mkemia Mkuu wa ile nchi anakuwa ndie mwenye uamuzi wa mwisho, bahati nzuri tumefanya mawasiliano na Mhe. Mwanasheria Mkuu juu ya suala hili na yeye akashauri kama vile ambavyo inavyostahiki kwamba maoni yanasikilizwa, kwamba sheria hii iongezwe kifungu kitakachotoa nafasi kwamba yule aliyekuwa hakutosheka ambae kwa upande wa pili. Mhe. Rashid Seif alisema kuna mtenda na mtendwa yaani yeye kamwita mmiliki, lakini ni vizuri tuelewe na wengine kwamba huyu mmiliki huyu anakuwa na kesi ya kujibu anaweza kuwa kaleta madawa ya kulevya, anaweza kuwa ndiye aliyenajisi.

Sasa huwezi tena ukamwambia na yeye umshirikishe kwenda kumuonyesha madawa yake ya kulevya katika uchunguzi ule, lakini hata hivyo inapofika Mahakamani akasema hakubaliani na maamuzi ya Mkemia Mkuu atakuwa na haki ya kufanya *reference* kwenye chombo cha juu, kwa hivyo Mhe. Mwanasheria Mkuu kasema tuongeze kifungu ambacho ni vizuri nikakisoma kutokana na maelezo yake, kwamba kuongezwe kifungu (5) na (3) Kinachosema endapo utatokea utatanishi au kwa sababu za msingi kutoridhishwa na matokeo ya uchunguzi wa Mkemia Mkuu, uchunguzi wa ziada unaweza kufanywa katika maabara inayotambulika ndani au nje ya Tanzania kwa kufuata utaratibu uliowekwa katika kanuni zitakazotungwa na Waziri kwa madhumuni hayo.

Sasa hapa suala linaweza likaja nani atalipia gharama lakini nadhani hiyo kanuni itakayotungwa inaweza kueleza nani atalipia gharama hizo, kwa hivyo kwa sababu ya utaalam wa kisheria wa Mwanasheria Mkuu hatukuwa na matatizo na suala hili.

Baada ya hapo Mhe. Salmin Awadh Salmin alizungumza suala la kwamba chombo kipewe fedha za kutosha kiwe na jingo lenye heshima, sisi pamoja na wale wengine waliosema hili tunakubaliana na hili, lakini hili tulisema ni suala la utawala zaidi kuliko kuliweka kwenye sheria. Ni suala la *management* na tumezingatia hayo hata Mhe. Hija Hassan Hija kasema hivyo hata Mhe. Ismail Jussa Ladhu pia kasema hivyo kwamba

kuwe na suala la wao kupata fedha za kutosha, ni kweli kidogo hali ya taasisi yetu ilivyo hivi sasa hairidhishi kwa hali halisi. Lakini baada ya sheria hii wizara itapata nguvu sasa kuweza kuiambia serikali kwamba tunaweza kulinda heshima yetu kupata chombo chenye maeneo yanayostahiki.

Mhe. Spika: Naendelea kuwaomba waheshimiwa wajumbe wanaotoka nje kwa dharura waelewe kwamba si muda mkubwa shughuli hii tunataka kuimaliza.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, kulikuwa na suala la Mhe. Rashid Seif kuna maneno Fulani aliyesema yatolewe kwamba kuna kifungu kile cha 9(4) kinachosema kama waziri atakavyotaka tukasema hilo sisi tunalikubali nalo lifanyiwe masahihisho, isionekane kwamba labda waziri ndio mwenye maamuzi ya mwisho.

Lakini suala la Mhe. Rashid Seif lililokuwa la msingi kuliko yale mengine madogo madogo ni lile la kusema ada anatoa nani, ada anatoa yule ambae analeta *sample* yake kuchunguzwa na kama utaisoma vizuri sheria kuna kifungu kimeeleza hivyo, kwamba ada analipa yule anayeleta *sample.* Kumekuwa na hoja kwamba pengine watu wanasema mchagua nyimbo ndio mlipaji, lakini kwa kawaida ada ya malipo inatumiwa taratibu kuna kitu ambacho kinaitwa *penalty and charges regulation* ambayo hiyo ndio ina *define* ukileta *sample* ya aina Fulani utalipa kitu Fulani, ukileta *sample* ya aina Fulani utalipa kitu Fulani.

Kwa hivyo ule mwana aliokuwa anauogopa Mhe. Rashid Seif unakuwa haupo kwa sababu hii inakuwa tayari imetungiwa kanuni na inajulikana, sasa tena ubinaadamu kama watakutana kichochoroni kwamba nitakupa hizi ili ufanye hivo hiyo itategemea na uadilifu kwa yule anayefanya.

Mhe. Rashid Seif naye vile vile masuala mengine yalikuwa ya utawala kwamba uwe na *organization structure* na kwamba Mkemia Mkuu aruhusiwe kuunda Idara kulingana na *sample* au haja ya taasisi, hili halina matatizo na kwa taarifa ya wajumbe ni kwamba tumeshafika *stage* hata kuchora ramani ya Idara gani ziwemo, zote zile zinazostahiki kuwemo katika afisi ya Mkemia Mkuu suala la idara gani iwemo litategemea na uwezo wa ile taasisi inavyokuwa, hata hizo taasisi za wenzetu hazikuamka tu siku ya tatu ikawa ina kila chombo. Ilijijenga taratibu ikaanza na zile idara za lazima halafu kila siku zilivyokwenda wakajijengea ukubwa kustahiki na mahtaji.

Mhe. Hija Hassan Hija yeye ni mjumbe alichosema tu kwamba kuna changamoto nyingi tunakubali kuna changamoto nyingi, akazungumza habari ya *contractor* na akachanganya taasisi zote kujengwa pamoja, mengine yapo nje ya uwezo wa Wizara ya Afya lakini tumejitahidi tumeomba majengo na tumepewa pale Maruhubi na la Bohari Kuu lipo pale, hata hayo ya Mkemia Mkuu tulitegemea kupewa pale tukenda tukasema hayatoshi serikali inazingatia kutupa ziada na ikiwezekana hata ile bodi ya madawa ingekuwa pale. Sote tukawa pale Baba mmoja Mama mmoja lakini sasa mengine hatuna uamuzi nayo katika kusema nini tupewe na nini tusipewe.

Mhe. Fatma Mbarouk Said yeye katuunga mkono lakini kubwaalilosema ambalo lilirudiwa na baadhi ya wajumbe ni kwamba haingefaa mjumbe yule wa chombo cha *chamber of commerce* awemo kwa sababu yeye ni mhusika, sisi katika suala ambalo lilikuwa linatupa tabu moja ni katika *system* tuliyokuwa tunatumia hivi sasa katika kushirikiana katika kuendeleza nchi hii kuna kitu kinaitwa BOT, kuna kitu kinaitwa PPP yaani *Public Private Partnership* sasa unapowaacha nje hawa hata jana Mhe. Ismail Jussa alikuwa anachangia hapa akasema kuna hatari siku hizi kuleta miswada tukawaacha wadau. Kuwaacha wadau maana yake ni wale watu ambao wana *interest* nayo, sasa hivi hatukuona vibaya kuwemo mtu kwenye bodi sio katika ile *management* ya utendji kwenye bodi ambayo ni bodi ya ushauri kupata maoni ya *private sector* ni vizuri zaidi kuliko kukaa nje wakawa wanalalamika hawana pakusemea kwa hivyo bado tunaona mjumbe yule ni vizuri kuwemo katika bodi.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu yeye kama nilivyosema mwanzo alikuwa na masuala mengine ya tafsiri ya lugha au tafsiri ya kizungu na Kiswahili, tunakubaliana nae katika kurekebisha na yote yale bila ya kupoteza muda takriban yote aliyoyashauri kuhusu lugha basi tunakubaliana nayo, kuna kifungu kile cha 3, 2,C kuna kifungu 4.2.C vyote vile tunakubaliana nae na kuna kifungu muda huu umezingatia.

Sasa suala la Mhe. Ismail Jussa Ladhu ambalo kidigo tunaomba kulitolea maelezo ni kwamba cheo cha Mkemia Mkuu awe na uzoefu angalau miaka mitano, yeye akasema ni mihaba sisi suala lililozingatiwa hata katika mjadala wa vikao vya serikali, tunasema tunalo hilo soko la kumpata mtu mwenye uzoefu wa miaka kumi na tukiwa hatuna maana yake tutapata dudu mtu lililo nje ya mazingira yetu na halafu tunaweza kulaumu kwamba tumemuajiri mtu ambae angekuwa lazima awe Mzanzibari, sasa tukatoa miaka mitano hii hata akiwa pale ataendelea kukomaa, ataendelea kujifunza na huyu tuliyenaye hivi sasa kwa mfano yeye ni *Doctor* ambae alikuwa na *lecture* Chuo Kikuu cha SUZA yeye ni *Chemistry by professional* kwa hivyo inawezekana hajawa na huo uzoefu wa muda mrefu kiasi hicho lakini baada ya kupewa taasisi hii na kwenda *short course* atajenga ule uwezo.

Sasa katika hiyo miaka inayokuja huko nadhani sisi tutakuwa hatupo wanaweza kuja kufanya marekebisho ili kumpata mtu mwenye uwezo mkubwa zaidi, kwa hivyo tunamuomba Mhe. Ismail Jussa Ladhu akubali kwamba kwa hali ya soko letu kwa hivi sasa hiyo ndio *level* iliyoweza kufikiwa, kuna mabadiliko ya kifungu cha kumi tunakubaliana nae, kuna mabadiliko ya kifungu cha kumi na nne tunakubali ushauri wake. Kwamba badala ya kumtafuta Mkemia Mkuu awe ndio Katibu tunakubaliana nae hilo lakini tunashauri kwamba tunahitaji mtu wa sheria ambae atakuwa anawasaidia wale wanapokwenda Mahakamani wawe na mtu anayeweza kuwasaidia, aiza itabidi tuajiri na bodi iwe na Mwanasheria wake au kwa hapa sasa turuhusiwe kumuingiza mjumbe kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu iwe ni mshauri mkuu katika mambo ya kisheria kwenye bodi.

Suala jengine lililokuja kwa Mhe. Subeit Khamis Faki amesema kitu *very interesting* anasema kwa nia njema huyu jamaa atakuwa anafanya kwa makusudi, lakini ukiisoma kwa kizungu inasema hukukusudia au kwa bahati mbaya kwa hivyo kile Kiswahili

alichokisema kwa kizungu ndio maana yake ile kwa nia njema, kwamba *in good faze* maana yake sikukusudia kufanya hivyo. Kwa hivyo hii hali ya nia njema inategemea kubahatika kwa sababu hii ni moja katika vitu vilivyokuwa vinafanya kwamba sikufanya makusudi.

Lakini Mhe. Spika, mtu anayefanya makusudi na asiyefanya makusudi akishafanya tu unamjua, kwamba utafanya mara moja sio makusudi, mara ya pili sio makusudi, mara ya tatu aa wewe unafanya makusudi. Lakini katika miaka minne au mitano hili sikukusudia Mhe. Spika, akija akikuripotia tu ile hali akija ukimuona tu unajua kwamba huyu anajuta kwa hili alilolifanya kwa hivyo ile *in good faze* iendelee kubaki.

Vile vile alitaka aingizwe Mjumbe kutoka vyombo vya ulinzi Mhe. Subeir Khamis Faki Ofisi ya Mkuu wa Mashitaka ni Mjumbe wa Bodi ambae yeye kwa jumla anakwenda *across* kwa *section* ya vyombo hivi, mara nyingi watu wa ulinzi ndio wanaoleta kesi za *sample* kuleta kwa Mkemia Mkuu, hasa Polisi, Usalama wa Taifa hata Jeshi yanapotokea matatizo hayo. Sasa kuna hatari ya kumtia mle ikawa balaa, kwa hivyo sisi tunashauri akiwemo yule Mkuu wa Mashitaka atakuwa amewakilisha vya kutosha masuala yanayohusu upande wa ulinzi.

Jengine ambalo amelisema ni kuomba labda waruhusiwe kununua vitu lakini kwa sababu hii Idara ya Serikali inabidi wafuate sheria kama inavyofanyika hivi sasa, kwa hivyo hakuna haja kufanya hivyo isipokuwa Idara itafuta taratibu zile zile zinazostahiki.

Mhe. Spika, sikutaka kuchukua muda zaidi kuna baadhi ya mambo sikuyasema moja moja lakini yamerudiwa hapa na pale, kama suala la Mhe. Rashid Seif alisema tuongeze kifungu tunakubali hicho kiongezwe hatuna matatizo, lakini badala ya kupoteza muda mrefu nikafanya kitu kimoja kimoja nimeona masuala haya yaliyokuwa mazito niyatolee ufafanuzi. Baada ya hapo niwaombe waheshimiwa Wajumbe waukubali waraka huu ili tukaufanyie kazi.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Basi niwahoji wanaokubaliana na hoja ya mswada huu wanyanyue mikono, wanaokataa, Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na Kukubaliwa)

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, sasa naomba kutoa taarifa kwamba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Baraza zima ili kuupitia Mswada kifungu baada ya kifungu na kuupitisha.

KAMATI YA BARAZA ZIMA

SEHEMU YA KWANZA

UTANGULIZI

Kifungu cha Kwanza	-	Jina fupi la kuanza kutumika
Kifungu cha Pili	-	Ufafanuzi pamoja na Marekebisho yake
Kifungu cha Tatu	-	Uanzishwa kwa Maabara pamoja na Marekebisho Yake
Kifungu cha Nne	-	Muhuri wa Maabara pamoja na marekebisho yake

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe kifungu kimoja kilipendekezwa na Mhe. Rashid Seif kwamba kiongezwe ambacho Mhe. Waziri pale amekubali, sasa ningeomba Mhe. Rashid tutakapofikia kifungu hicho akumbushe ili kifungu hicho kipate ufafanuzi ni kifungu gani ambacho makubaliano yao yapo kati ya maoni na Mhe. Waziri aliyejibu.

Kifungu cha Tano	-	Kazi za Maabara pamoja na marekebisho yake

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Mwenyekiti, hapa.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Rashid Seif hapa alitaka tuweke kifungu chengine na tunakubali Mhe. Mwenyekiti.

Kifungu cha Tano	-	Kazi za Maabara pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha Sita	-	Kushirikiana na taasisi nyengine
Kifungu cha Saba	-	Siri ya Matokeo ya Uchunguzi pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha Nane	-	Uteuzi wa Mkemia Mkuu wa Serikali
Kifungu cha Tisa	-	Wajibu na uwezo wa Mkemia Mkuu wa Serikali pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu cha Kumi	-	Wachunguzi wa Kemikali pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha Kumi na Moja	-	Kazi za Mchunguzi wa Kemikali pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha Kumi na Mbili	-	Wafanyakazi wengine pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha Kumi na Tatu	-	Kinga kwa wafanyakazi pamoja na marekebisho Yake
Kifungu cha Kumi na Nne	-	Bodi ya Ushauri pamoja na marekebisho yake

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, jana Mhe. Ismail Jussa Ladu alipokuwa akichangia alizungumzia kuhusu kifungu cha kumi na nne kifungu kidogo cha nne kuhusiana na uteuzi wa katibu wa Bodi, alipendekeza kwamba ni vyema Mkemia Mkuu mwenyewe ndio akawa katibu wa Bodi, nimemsikiliza Mhe. Waziri alipokuwa akifanya majumuisho hapa alikubaliana na mapendekezo haya.

Lakini mimi nadhani kuna mambo mawili kwanza suala la katibu wa bodi kwa tunavyoelekea hasa katika kuimarisha hivi taasisi ni *specialization* maalum yaani ndio maana kuna taasisi zinazowafunza watu hawa mpaka mtu anafikia kuwa *chartered*

secretary maana yake ni mtu ambae alifunzwa kuwa Katibu wa chombo kama hichi na kuweza kukitumikia kwa vizuri.

Jengine ni kwamba si vyema kwa kweli kwa hii kada kila mtu tu akawa katibu kwa mfano Mkemia Mkuu taaluma yake ni Mkemia, mwengine ni *engineer* na mwengine sijui ana taaluma gani, sasa hizi kazi za kuwa katibu wa Bodi zina utaalam wake maalum.Kwa hivyo mimi nilidhani kwamba kufanya Mkemia Mkuu kuwa ni Katibu wa Bodi na ukitizama pia hata kwa hadhi yake na kwa msaada ambao anaweza kuutoa kwa bodi yenyewe si vyema yeye akawa katibu wa Bodi, lakini nadhani hiki kifungu kibaki kama kilivyo kwamba bodi yenyewe iteue mtu mwenye taaluma iliyotajwa ili aweze kuwa katibu wa bodi.

Kwa hivyo mimi nilikuwa nashauri tubaki na hiki kifungu kama kilivyo badala ya Mkemia Mkuu kuwa ni Katibu wa Bodi.

Mhe. Spika: Kwa hivyo katibu wa bodi tunakubaliana kwamba awepo lakini asiwe Mkemia Mkuu wa Serikali, kulitajwa na mjumbe mmoja hapa katika kifungu hiki kwamba atateuliwa na Mhe. Waziri na nadhani tulipata majibu hebu Mhe. Waziri weka vizuri juu jambo hili.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti sisi tulikuwa na mawazo hayo kumuona kwamba Mkemia Mkuu awe mbali na Katibu awe mbali, ndio maana tukasema kama lazima Mkemia awe Katibu itabidi apatikane Mwanasheria hata kama ni Mjumbe kuotoka kwa Mwanasheria Mkuu ili aweze kusaidia kazi, lakini kama atafanya kazi za ukemia halafu na ukatibu. Lakini Mhe. Ismail Jussa Ladhu alisema huyu ndio anayeyajua yale mambo yote na inabidi ayawasilishe pale kama anavyoweza kuyawasilisha, sasa tukaona kwa manaa hiyo kama itawezekana sawa, lakini kutokana na ushauri wa Mwanasheria na nafikiri tumshauri na Mhe. Ismail Jussa Ladhu kwamba lazima aweko katibu.

Halafu nakumbuka kuliomba awepo mjumbe kutoka Wizara ya Wanawake na Watoto awemo humu ili nae aweze kutoa taarifa zinazotokea kwenye matatizo ya kubakwa na athari za kinamama, kwa sababu mwisho inafika huko kwa Mkemia Mkuu, kwa hivyo na yeye atakuwa na ushuri na sisi hatukuwa na pingamizi.

Mhe. Spika: Kwa hivyo tunachokubaliana hapa ni kwamba Mkemia Mkuu wa Serikali abakie kama mjumbe na katibu awe mtu mwengine na awe Mwanasheria na mwengine atoke Wizara ya wanawake na watoto.

Kwa hivyo katibu atoke Afisi ya Mwanasheria Mkuu au Mwanasheria. Vile vile kuwa na mjumbe kutoka Wizara ya Wanawake na Watoto. Ndiyo marekebisho tunayoyafanya hapa. Tunakubaliana na hilo.

Mhe. Jussa: Mhe. Mwenyekiti, kwanza ambalo amelizungumza Mhe. Mwanasheria Mkuu naomba nikubaliane na yeye. Jana nilipata nafasi nzuri ya kushauriana na yeye na

alinitosheleza kwa hoja. Kwa hivyo na mimi nikipewa hoja Mhe. Mwenyekiti, huwa nina kawaida ya kuwa msikivu sana. Kwa hivyo nilipokea pendekezo lake na naliunga mkono.

Pili ingawa kuwa sikulitoa mimi lakini nataka kulisaidia Baraza lako lisije likafanya makosa. Kilichopendekezwa jana Mhe. Mwenyekiti ilikuwa kama ilivyotajwa Mkurugenzi wa Mazingira na Mkurugenzi mwenyedhamana ya biashara. Alipendekeza atajwe *specifically* Mkurugenzi wa Ustawi wa Jamii, kwa sababu tukisema wizara tu ni kubwa. Ilitajwa *specifically* katika mapendekezo yaliyotolewa hapa kwamba awe ni Mkurugenzi wa Ustawi wa Jamii. Nadhani kama sikosei ilikuwemo katika mapendekezo ya Kamati ambayo yaliwasilishwa hapa.

Mhe. Spika: Kwa hiyo tunakubaliana kwamba Mkemia, Mkuu wa Serikali anabakia kuwa ni Mjumbe, Katibu awe ni Mwanasheria. Na vile vile nafasi ya Mkurugenzi Mwenye dhamana ya biashara nafasi yake tunaongezea, huyu anabaki na tunaongezea na Mtu wa Ustawi wa Jamii.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, huyo wa biashara na wakulima anabaki na anaongezwa Mkurugenzi wa Ustawi wa Jamii.

Kifungu cha 14	Bodi ya Ushauri Pamoja na Marekebisho yake
Kifungu cha 15	Muda wa Wajumbe Pamoja na Marekebisho yake
Kifungu cha 16	Vikao vya Bodi
Kifungu cha 17	Mwenendo wa Vikao vya Bodi
Kifungu cha 18	Kazi za Bodi Pamoja na Marekebisho yake
Kifungu cha 19	Kamati Pamoja na Marekebisho yake
Kifungu cha 20	Malipo kwa Bodi

SEHEMU YA TATU - MASHARTI YA FEDHA

Kifungu cha 21	Fedha na Rasilimali Pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu cha 22	Bajeti
Kifungu cha 23	Ukaguzi wa Hesabu Pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu cha 24	

Mhe. Ismail Jussa: Mhe. Mwenyekiti, naomba nijitosheleze. Kwamba katika mchango wangu jana nilipendekeza kile kifungu cha 24 (2) chenye maelezo ya kufungia yanayohusu adhabu, imewekwa isiyopungua. Nikapendekeza ama iwekwe isiyozidi au iwekwe *maximum* na *minimum*. Katika maelezo ya Mhe. Waziri alipokuwa anatujibu sikubahatika kulisikia hili. Hebu naomba anisaidie ili tuelewe tunapitisha nini Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Afya: Mheshimiwa tumekubali hilo, kwenye marekebisho ya Kamati waliweka *minimum* huku walikuwa wameikuta. Sisi tunakubali kwamba na huku juu nako kuwekwe *maximum* ili kutoa nafasi ya mtu kumkomoa mwenzake. Tunakubali hilo.

Kifungu cha 24	Makosa na Adhabu Pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu cha 25	Kanuni Pamoja na Marekebisho yake

Kifungu cha 26 Kufutwa Kwa Sheria ya Chakula na Dara Sura ya 78 na Kubakiza.

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Baraza Zima umeupitia Mswada wangu kifungu kwa kifungu na kuukubali pamoja na marekebisho. Sasa naliomba Baraza lako Tukufu liukubali. Naomba kutoa hoja.

(Hoja imetolewa iamuliwe)

(Hoja imeamuliwa na kuafikiwa)

Mswada wa Sheria wa Kuanzisha Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali ya Mwaka 2011

(Kusomwa kwa mara ya pili)

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, naomba kutoa hoja kuwa Mswada wa Sheria wa Kuanzisha Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali ya Mwaka 2011 usomwe kwa mara ya pili. Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

(Hoja imetowa iamuliwe)
(Hoja imetolewa na kukubaliwa)

Katibu: Mhe. Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Mswada wa Sheria wa Kuweka Masharti ya Kuanzisha Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali Pamoja na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo, sasa umepitishwa rasmi na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

Naomba kutoa taarifa kwamba shughuli zote tulizokusudia siku ya leo zimekamilika.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, nichukue nafasi hii kukushukuruni kwa kumaliza shughuli zote zilizopangwa kwa siku ya leo. Kwa maana hiyo jioni hatuna shughuli ya kufanya, isipokuwa kupungumzika na wengine kuendelea na shughuli zao.

Kabla ya kuahirisha shughuli zetu naomba nitoe tangazo moja. Nimetumwa na Mnadhimu ya Upande wa CUF nitoe taarifa kwamba wajumbe wote wa upande wa CUF wabaki baada ya kuakhirisha Kikao hichi. Kuna mambo muhimu ya kuzungumzwa. Na mimi nakubali ukumbi wautumie sisi tukiondoka.

Baada ya hayo basi Waheshimiwa Wajumbe nakushukuruni tena kwa kazi nzuri mliyoifanya. Sasa naahirisha Kikao hichi hadi tarehe 17/10/2011, siku ya Jumatatu, saa 3:00 za asubuhi.

(Saa 6:40 mchana Baraza liliakhirishwa hadi tarehe 17/10/2011 Saa 3:00 Asubuhi)